

NJIA ILIYOWEKWA NA MUNGU

YA KUUENDEA USHIRIKA



Baba yetu wa Mbinguni mwenye Neema, kweli sisi ni watu waliojaliwa usiku wa leo, hata tunaweza kuutazama uso Wako na kukuita Baba yetu. Tukijua haya, ya kuwa tumepita toka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu tumemwamini Mwana wa pekee. Na kupitia kwa mateso Yake, na kufa, na naam, kufufuka tena apate kuishi milele, tuna Uzima wa Milele kupitia imani hii katika Yeye.

² Na kuna mambo mengi maishani mwetu ambayo si sawa kabisa. Sisi ni watu wanaotembea gizani katika ulimwengu huu, kwa ile Nuru tu tunayoweza kupata kutoka Mbinguni, tukitembea katika ulimwengu wenye giza, tukitembea katika Nuru wakati Nuru ikiangaza katika njia zetu. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Nuru ya Mungu itamulika sana kwenye njia zetu, hata tutaweza kuwa nuru inayoangaza kwa wengine, wapate kuiona Injili tukufu ya Bwana Yesu, na waingie kwenye ushirika huu mkuu. Tujalie, Bwana.

³ Tusamehe dhambi zetu nyingi na makosa, dhambi zetu za makosa, na lolote baya tulilofanya ama kusema, tunakuomba kwa unyenyekevu, Baba yetu, utusamehe. Nasi tunaomba ya kwamba Roho Wako Mtakatifu atakuja usiku wa leo katika nguvu kuu, amwagwe juu ya kusanyiko hili na atatimiza kila hali tunayohitaji usiku wa leo. Na jalia turudi kwenye makazi yetu usiku wa leo, wenye furaha, tukishangilia, tukikusifu Wewe. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Bwana Yesu, Mwokozi wetu. Amina.

⁴ Mwaweza kuketi. Ni majaliwa kurudi hapa kwenye jumba la mikutano tena usiku wa leo. Tulikuwa na wakati mzuri sana kwenye kiamshakinywa cha wahudumu asubuhi ya leo, ushirika mkuu ambao Bwana alitupa. Nasi tulikuwa tukitazamia ibada ya kesho, naamini ni alasiri, sivyo, ndugu? Saa nane na nusu, kesho alasiri.

⁵ Na kesho alasiri, nilifikiri kwa kuwa ni Jumapili ungekuwa ni wakati mzuri wa kuwaombea wagonjwa tena kesho alasiri. Labda kungekuwa na watu ambao wangekuwa wametoka kazini, na wangepata kuwaleta wapendwa wao humu. Na labda nafasi pekee ambayo wangekuwa nayo ya kuja ingekuwa katika ibada ya—ya alasiri. Kwa hiyo hao wavulana watakuwa wakigawa kadi za maombi yapata saa saba na nusu basi, ama saa nane kasorobo.

⁶ Kama unataka kadi ya maombi, njoo upokee kadi yako ya maombi karibu saa nane kasorobo, nadhani. Yoyote... Msifanye hivyo baadaye sana, ninyi mnaotaka kadi ya maombi, njoni. Halafu basi hiyo haitakatiza ibada zingine, na ndipo tunaweza kuanza hasa kwenye saa nane na nusu.

⁷ Sababu ya sisi kufanya jambo hili ni kwamba sisi... halikatizi mikutano yoyote, ibada mahali pengine popote. Huenda ikawa kuna wageni hapa. Nina marafiki fulani jengoni mahali fulani walio hapa, ninajua wako mkutanoni, Ndugu Fred Sothmann, na wengi wa marafiki zangu kutoka Canada, nami nasikia ya kwamba Ndugu Norman yuko hapa mahali fulani kutoka huko chini Phoenix, Arizona, na kadhalika, ama, Tucson, Arizona.

⁸ Na kuna makanisa, makanisa mazuri hapa, basi chagua kanisa upendalo, mahali fulani ukahudhurie ibada kesho, hakika mtakaribishwa sana. Nami ningependekeza hawa ndugu wa Full Gospel ambao wanaudhamini mkutano huu. Watu hawa wanaamini Injili ya namna hii, la sivyo wasingeniruhusu hapa. Na kwa hiyo, tunawapendekeza kwenu, basi waendeeni, muwasikilize, watawafaa.

⁹ Na sasa, ndipo kesho si zaidi ya saa nane na robo, hao wavulana watakuwa wakigawa kadi za maombi. Halafu, tutafanyiza mstari wa maombi mara baada ya ujumbe na kuwaombea wagonjwa tena.

¹⁰ Basi ni wangapi wanaofurahia huu mkutano? Loo, hilo ni sawa tu. Ni wangapi hawakuwa katika mmojawapo wa mikutano hapo kabla? Hebu tuone mikono yenu, kamwe hamjahudhuria mmoja wa hii mikutano. Loo, jamani, nusu ya wasikilizaji, hawajawahi kuwa katika mmojawapo hapo kabla. Vema, tunatumaini ya kwamba mtarudi na kuwa pamoja nasi. Tunaninii tu, tukizungumzia asubuhi ya leo ninii, mmoja wa nyakati nzuri sana za ushirika tuliokuwa nao asubuhi ya leo kwenye meza ya kiamshakinywa pamoja na wahudumu hawa na wake zao, na marafiki kutoka mjini na karibu na hapa, wakati mzuri sana. Ninapenda tu ushirika, napenda tu wakati huo mzuri sana.

¹¹ Na sasa, juma lijalo lote, kila jioni wakati uo huo, saa moja na nusu, tunatarajia... Kila mtu anayeweza, waleteni wapendwa wenu na mje, nitajaribu nisichelewe sana. Kamwe hatutatangaza chochote, kwa sababu ninaamini kwa moyo wangu wote katika kuongozwa na Roho Mtakatifu, lolote Yeye asemalo tufanye, tunalifanya tu, bila kujua wakati mmoja kuanzia mwingine kile tutakachofanya.

¹² Nimeenda jukwaani mara nyingi, nikiwazia, "Vema, nitaanzisha somo," ninachukua somo fulani, nitaanzia katika Ufunuo na kuishia katika Mwanzo, ama vinginevyo, popote tu ninapohisi Roho akiongoza. Ninaamini ya kwamba wana na

binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu, mnaona, wanaongozwa kiroho.

¹³ Na loo, jinsi ningetaka kuona uamsho mkuu ukitokea katika bonde hili dogo hapa! Loo, jamani! Liwe tu utukufu wa Mungu hapa ambapo hata magazeti, na televisheni, na chochote kile kisingeweza kunyamaza. Umwache Mungu aanze kutembea miongoni mwa watu Wake, tuache kila mtu aliye hapa usiku wa leo ajifungie tu ndani pamoja na Mungu, kila mtu hapa atajua habari zake hivi karibuni. Hakika huwezi... Ni kama tu kujaribu kuzima moto kutoka...kutoka kwenye nyumba kwenye upepo mkali, ni ninii tu, huwezi kuuzuia. Wakati Roho wa Mungu anapoanza kuupulizia moto huo, jambo fulani hutukia.

¹⁴ Nimesafiri kote ulimwenguni, na nimeona watu wa kila namna, na baadhi yao hata hawajui mkono wa kulia au wa kushoto ni upi, nimewaona watu ambao hata hawakujua mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, na hata hivyo, kamwe hawakusikia Neno la Bwana Yesu maishani mwao mwote, na hata hivyo wanapompokea Roho Mtakatifu, wanatenda sawasawa kabisa na vile mtendavyo mnapompata. Hata hawajui mkono wa kulia wala wa kushoto, bali wanapompokea Roho Mtakatifu, wanafanya jambo lile lile mnalofanya, na kutenda vivyo hivyo tu.

¹⁵ Kwa hiyo ni baraka ya kawaida kwa watu wote, wawe ni Wayahudi, Wakatoliki, au Waislamu, Budha, Kalasinga, Mjaini, ama wowote wale. Wao ni... Ni kwa yeyote atakaye.

¹⁶ Kidogo niliwataja hao karibu pamoja, *Kalasinga* na *Jaini*, hizo ni dini mbili tofauti za India. Makalasinga ni wale wanaobeba kisu kitakatifu nyweleni mwao, na Wajaini ndio wale wanaoamini katika kuzaliwa upya katika mwili mwingine, ambao hufagia barabara wanayoipitia, kama wakikanyaga maskini chungu ama mdudu huenda ikawa ni baadhi ya jamaa zao ambao wamerudi. Na, loo...

¹⁷ Nilikaribishwa alasiri moja nilipoenda Bombay, ambako ninaamini mimi, kwa neema ya Mungu, nilihubiria kusanyiko kubwa zaidi, lililokadiriwa kuwa watu laki tano kwa wakati mmoja. Nami nilikaribishwa alasiri hiyo na dini kumi na saba mbalimbali, na kila moja ya hizo ilimkana Yesu Kristo. Hmm! Hizo ni ninii... Dini kumi na saba mbalimbali, yapata nane ama kumi kati yao walipata kuzungumza, lakini kila mmoja alikuwa akisimulia jinsi Ukristo ulivyokuwa duni, na jinsi ulivyokuwa mbaya, na jinsi ulivyotiwa alama, ndipo ni—nikajisikia kana kwamba ningekuwa msaliti kwa Kristo kama ningalinyamaza, kwa hiyo si—sikunyamaza.

¹⁸ Na kwa hiyo, usiku huo, walipokuwa wakizungumza pale, na hapo walisimama maraja kwenye mito yao, na—na watu wote watauwa, na watu watakatifu, na wa namna mbalimbali,

ndipo wakati Roho Mtakatifu alipoanza kutenda kazi, nilimwona kipofu amesimama pale. Wala kamwe hajaninii... Akamwambia, kasema, “Umekuwa kipofu karibu maisha yako yote, kwa sababu wewe ni mwabudu jua, uliangalia jua na macho yako yakapofuka.”

¹⁹ Wanafikiri wataenda Mbinguni, lakini hiyo ndiyo adhabu yao inayowabidi kulipia. Nena kuhusu ushika sheria! Nao inawabidi kulipa gharama hiyo ya kulitazama jua mpaka wanakuwa vipofu.

²⁰ Kamwambia alikuwa ombaomba, alikuwa na mke na watoto wawili, mvulana mmoja miaka tisa, huyo mwingine kumi na mmoja. Hayo yote yalikuwa kweli. Jina lake, hata nisingeweza kulitamka, ilinibidi kutaja tahajia za maneno hayo, sawa kabisa, jinsi Roho Mtakatifu alivyolitoa, kama tu anavyofanya hapa usiku, na kadhalika. Yeye daima yu sahihi kabisa, kamwe hakosei; hawezi kukosea na awe Mungu, haina budi kuwa sahihi wakati wote.

²¹ Na kwa hiyo, walidhani ilikuwa, labda... Ungeweza kulishika likitoka kwa wasikilizaji, nami hufanya hivyo mara nyingi. Wanafikiri ni telepathia, na hata hivyo watasema, “Bwana asifiwe!” Lakini hata hivyo, hawa—hawaamini hilo kabisa moyoni mwao, mnaona. Dhamiri yako ya ndani hunena kwa sauti kubwa kuliko kinywa chako kifanyavyo, unaona, wakati huo. Ni dhamiri yako ya ndani, kile unachowazia hasa, hicho ndicho Roho Mtakatifu anashika na kufunua. Ndipo basi wakati...

²² Mnaamini hilo? “Yesu aliangalia wasikilizaji na kutambua mawazo yao.” Hiyo ni kweli. Vema.

²³ Kwa hiyo basi, wao... Mtu huyu akisimama pale, kipofu, macho yake meupe kama shati langu. Nikaangalia nyuma, nikasema, “Bila shaka hayo yote ni kweli, kama vile huyu mtu anavyoshuhudia.” Lakini nikasema, “Hakuna kitu ningaliweza kufanya kumsaidia, ni kumwomba tu.” Nikageuka na kuangalia tena, na hapo nikamwona amesimama kama kivuli juu ya mahali alipokuwa amesimama hapa, hapo katika ono alikuwa akiangalia huku na huku, akicheka, huku ameinua mikono yake. Loo, jamani, hakuna kitu kitakachouzia basi. Ibilisi asingeweza kutoa pepo wa kutosha kuzimu kuukomesha. Mungu tayari ameonyesha jambo hilo, ni BWANA ASEMA HIVI basi. Hakuna kitu, hakuna kitu kinachoweza kuuzua.

²⁴ Halafu una wasikilizaji mikononi mwako, unaona. Unajua kile unachozungumzia, nisingethubutu kulisema kama sikujua nilichokuwa nikisema. Nami nilikuwa nimeona lile ono, nilijua Bwana alikuwa ananda kumponya. Ndipo mimi... Bwana akanipa hilo jukwaa basi.

²⁵ Nikasema, “Hakika nilikuwa na wasiwasi sana alasiri ya leo nilipokuwa huko chini kwenye hekalu la Jaini na wakati dini

kumi na saba mbalimbali, waliniambia, zilikuwa zimekusanyika pale, na, huku nikijiandaa kwa ajili ya mkutano huu ujao. Nao wakaniambia jinsi Ukristo ulivyokuwa duni, na jinsi tulivyokuwa na ibada ya mwanadamu, na ati tulimwabudu mwanadamu, wala haikuwa hivyo.” Nami nikasema, “Waislamu hapa walisema walikuwa na dini iliyo kuu kuliko zote, wala hapakuwapo na kitu kikubwa ulimwenguni kama dini yao ilivyokuwa, walianza kabla ya Mwanzo wetu, ama kadhalika.” Na—nami nikasema, “Mambo haya yote . . .”

²⁶ Nami nikasema, “Wala msifikiri kwamba sijui mnachowazia, mnaifikiri ni telepathia.” Nami nikasema, “Mtu yeyote ambaye kweli angejua telepathia anajua hiyo ni tofauti. Telepathia ni kitu fulani, unasema tu yale hao jamaa wengine wanayosema.” Nami nikasema, “Vema, hilo ni—hilo ni kosa. Jinsi ingefunua dhambi na mambo yaliyofichika ya moyoni?” Mnaona, watu huchukua tu uamu, na kuliweka pale, na kuendelea, hayo tu ndiyo wanayojua kulihusu.

²⁷ Nikasema, “Lakini ingewezaje kufunua mambo yaliyofichika moyoni mwao ambayo hawajayawazia kwa miaka mingi ambayo imepita? Mtu yeyote angejua hilo halikuwa na uhusiano wowote na telepathia.” Lakini nikasema, “Huyu hapa mtu amesimama, naye ni mwabudu jua.” Nikasema, “Mngefanya nini sasa? Kama mngekuwa mmesimama hapa, ninyi Waislamu, mngemwambia kwamba alikuwa amekosea, aliabudu kiumbe badala ya Muumba.”

²⁸ Waislamu ni watoto wa Ishmaeli. Tunajua ya kwamba wanamwamini Mungu yeye yule tunayemwamini, bali wanaamini ya kwamba Muhammad alikuwa nabii Wake; tunaamini kuna Mungu mmoja wa kweli na aliye hai na Yesu ni Mwanawe, Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

²⁹ Hawaamini . . . Kasisi wa Kiislamu aliniambia, kasema, “Na iwe mbali na Mungu kuwa na mwana, Roho kuwa na mwana.” Mnaona jinsi giza linavyoingia kwao?

³⁰ Kwa hiyo basi, nikasema, “Vema, huyu hapa mtu amesimama sasa. Kama hii ni telepathia, sijui chochote kuihusu; kama hii ni saikolojia, sina elimu ya darasa la saba. Kwa hiyo, ninyi jamaa mlio na Ph.D. zenu, nanyi watu mnaofahamu telepathia, nanyi watu ambao ni watu watakatifu, ninyi Waislamu, na ninyi Makalasinga, na Wajaini, na ninyi nyote leo mlioupa Ukristo changamoto, ninawapa changamoto katika Jina la Bwana Yesu Kristo mje myafumbue macho ya huyu mtu, ikiwa dini yenu ni kuu hivyo.” Nikasema, “Hakika, kama kuna . . . Mtu fulani hana budi kuwa sahihi, na mtu fulani hana budi kuwa amekosea.”

³¹ Hiyo ni kweli. Kamwe usiogope kuuweka Ukristo kwenye shindano la kuamua; Mungu ni halisi, la sivyo Yeye si Mungu. Kuna dini moja tu ya kweli, na hiyo ni Ukristo. Sasa, huwezi kuuigiza, huna budi kujua unachozungumzia, nawe huna budi

kujua ya kwamba Mungu amekwambia ufanye hivyo, la sivyo kamwe halitafanikiwa. Unaona? Wala nisingalisema hilo bure kama sikuwa nimeona ono kwamba lilikuwa linaenda kutukia.

³² Kama tu ninavyomwazia Eliya juu ya Mlima Karmeli, kamwe asingaliwacheka hao manabii, na makuhani, na kadhalika, isipokuwa angekuwa... Alisema, "Bwana, nilifanya haya yote kwa amri Yako." Bwana alikuwa amemwonyesha la kufanya.

Yesu alisema, "Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe kwanza."

³³ Kwa hiyo, nilikuwa nimeona pale ya kwamba mtu huyu alikuwa anaenda kufunguliwa macho yake. Nikasema, "Mngefanya nini? Mngefanya nini? Alisema ya kwamba atamtumikia Mungu atakayeyafungua macho yake." Nikasema, "Sasa, ninyi Waislamu mngemwambia alikuwa amekosea, nanyi Wabudha mngewaambia Waislamu walikuwa wamekosea. Mngefanya nini? Mngabadilisha tu njia yake ya kuwazia."

³⁴ Nikasema, "Saikolojia," nikasema, "tuna kitu kile kile Marekani, Wabaptisti wote wanataka kuwafanya Wamethodisti wote Wabaptisti, na—na Mmethodisti anataka kuwafanya Wapentekoste wote Wamethodisti, nao Wapentekoste wanataka kuwafanya wote Wapentekoste. Ni kitu gani? Ni kumbadilisha kimawazo, saikolojia yote."

³⁵ Nikasema, "Lakini tuna Mungu mmoja tunayemwabudu, njia mbalimbali tu za kuabudu." Nikasema, "Lakini kwa kweli, Yehova Mungu wa halisi wa kweli, aliyemfanya mwanadamu... Nami nasema alikosea, alikiabudu kiumbe badala ya Muumba, hiyo ni kweli, lakini sasa, kama amekosea na anataka kusahihishwa, na kumrudia Muumba halisi, hebu huyo Muumba halisi ayafungue macho yake apate kuwa wa manufaa Kwake." Nikasema, "Sasa ninawapa changamoto ninyi nyote mje jukwaani mkamfungue macho."

³⁶ Kulikuwa kimya kuliko ilivyo hapa sasa, zaidi ya watu laki tano. Hujawahi kusikia... Walikuwa wamelundikana tu, na kadiri ungeweza kuona ni kundi moja kubwa, jeusi la watu.

³⁷ Nikasema, "Mbona mmenyamaza hivyo? Alasiri ya leo mlikuwa mkielezea jinsi Ukristo ulivyokuwa duni, jinsi usivyokuwa na nguvu, na jinsi ulivyogawanyika katika madhehebu mbalimbali." Nikasema, "Sasa njoni, hebu tuone kile dini yenu inachoweza kumfanyia." Wala hakuna mtu aliyesema neno.

³⁸ Nami nikasema, "Bila shaka hamji, kwa sababu hamwezi." Nikasema, "Sasa, ninyi Waislamu mnaona, hao hapo makasisi wote wa Kiislamu, na kadhalika," nikasema, "kila mtu yuko kimya." Ndipo nikasema, "Fursa iko wazi, njoni moja kwa moja huku juu mkamfungue macho yake. Na mkiyafungua, nitamwamini mungu mnayemtumikia."

³⁹ Nikasema, “Kwa sababu hamwezi kufanya hivyo, wala na mimi siwezi, bali Mungu wa Mbinguni, aliyemfufua Mwanawe, Yesu Kristo, amemtuma Roho Wake, na Roho Wake anatenda kazi kupitia Kanisa Lake kufunua siri za moyo. Na kutoa dai halisi la kinabii kwamba Kuja Kwake kumekaribia, wakati makosa yote yangerekebisha, Yeye, Bwana Yesu, amenionyesha ono ya kwamba mtu huyu atapata kuona.

⁴⁰ “Kama hatapata kuona, mimi ni nabii wa uongo na ninapaswa kufukuzwa India. Lakini kama akipewa kuona mnawajibika kwa Mungu kuyasalimisha maisha yenu kwa Yesu Kristo, maana huyo hapo kasisi wenu, hao hapo makuhani wenu wote wa Kibudha, na makasisi wenu wa Kiislamu, na makasisi wenu wengine wote wameketi tu kimya, nao wanaogopa kukabiliana nalo.”

⁴¹ Nikasema, “Kwa hiyo basi ningekuwa vivyo hivyo, lakini Bwana ameonyesha ono kwamba atapata kuona. Sasa hebu Mungu aliye Mungu kweli anene.”

⁴² Wakamleta huyo mtu karibu. Hawayafasiri maombi. Nikasema, “Bwana Mungu, Wewe ni Mungu tu leo kadiri ulivyowahi kuwa, Nawe umeonyesha ono hili kwamba mtu huyo angepata kuona. Sasa hebu mtu huyu apate kuona, katika Jina la Bwana Yesu.”

⁴³ Mara tu niliposema hivyo, alipiga mayowe na kunishika kwa nguvu, akakimbia, meya wa jiji alikuwa ameketi pale, mara akamshika, watu wakaanza kupiga mayowe. Huo ulikuwa ndio mkutano wa mwisho ambao ningeweza kufanya huko India. Wao...Ilinibidi kuondoka. Mbona, hata walirarua mifuko ya koti langu, wakati wanamgambo mia tatu ama mia nne wakijaribu kuwazuia kwa fimbo. Wangewakanyaga hao askari, waingie chini yao namna hiyo, wakijaribu kukugusa, walivua viatu kutoka miguuni mwangu. Na kwa zaidi ya saa mbili nilikuwa nikipitia kwenye umati wa watu nikiwa ndani ya gari, huku askari wakijaribu kuwasukuma nyuma na kadhalika, watu wakiona njaa na kiu.

⁴⁴ Ni kitu gani? Mungu yeye yule aliyekuwako daima, atakuwako sikuzote, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Usiugope Ukuzote, bali hakikisha unajua unachozungumzia. Unaona, kuwa na uhakika ya kwamba Mungu alikutuma, Mungu amekuonyesha, na kukwambia dhahiri. Kama akikwambia ufanye jambo fulani, usiugope, nenda ukalifanye, maana Mungu alisema ulifanye.

⁴⁵ Ni wangapi waliokuwa Portland wakati ule ambapo yule mwendawazimu alikimbia jukwaani kuniua? Je, yeyote wao angali hai hapa? Mchungaji hapa alikuwapo, alikuwa akiniambia leo. Sasa, kuna wakati ni heri ujue unachozungumzia. Mtu huyo, mara mbili, mara tatu ya ukubwa wangu, mwendawazimu, amerukwa na akili, aliniambia,

akasema angevunja kila mfupa mwilini mwangu, na kujaribu kunitemea mate usoni, na kadhalika.

⁴⁶ Nami nikaketi tu...Mbona, hakuna kitu ningaliweza kufanya, ni kusimama tu na kumwangalia. Na papo hapo Roho wa Bwana akaanza kunena, na kusema, “Kwa sababu umemwasi Ro—Roho wa Mungu, utaanguka juu ya miguu yangu usiku wa leo.”

Akasema, “Nitakuonyesha nitaangukia miguu ya nani!” Akarudisha nyuma ngumi hiyo kubwa namna *hiyo* apate kunipiga.

Kamwe sikuinua sauti yangu, nilisema, “Shetani, toka ndani yake.”

⁴⁷ Akazunguka na kuanguka miguuni mwangu, yale hasa Bwana aliyosema angefanya. Hiyo ilikuwa ni huku kwenu. Mkosoaji fulani, si muda mrefu uliopita, aliyeongolewa na hilo, aliita kikosi cha polisi, na wangali walikuwa nalo kwenye kumbukumbu huko Portland, Oregon. Hiyo ni kweli.

⁴⁸ Vema, na huko Afrika, wachawi, na kila kitu, husimama na kutoa changamoto. Ujerumani, nilikuwa na wachawi kumi na watano kila upande wamesimama, huko Ujerumani, wakisema ale maneno makuu, na kukata manyoya na kujaribu kurusha uchawi, na kusababisha wi—wingu. Ndugu, dada, wakati mwingine hamwelewi hapa Marekani ambapo kila kitu kinapendeza tu, hujui utakutana na nini ukifika kule.

⁴⁹ Nao umati huo wa watu thelathini ama arobaini elfu umeduwaa kabisa nalo hema likitikisika namna hiyo, wao wameketi pale wakipindua vitu hivi vyote na kupitia kwa uchawi wao, wakinirushia uchawi, kwa sababu nisingewapokea, tena niliwaambia walikuwa wa ibilisi.

⁵⁰ Wakati tu tulipokuwa tumesimama pale, nikijiandaa kufanya wito wangu wa madhabahuni, walisema wangeita hiyo dhoruba, nao wakaiita. Ndugu Arganbright, nafikiri huenda akawa hapa usiku wa leo, kama hakuwa, atakuwa kwenye mkutano ujao, alikuwa ameketi moja kwa moja jukwaani, akasema, “Vipi kuhusu hilo?”

⁵¹ Nikasema, “Keti tu kimya na uombe; inanibidi kungojea nione yale Yeye asemayo.” Katika dakika chache tu, nikaanza kumhisi huyo Roho Mtakatifu akianza kutenda kazi. Loo, jamani, ni hisia ya jinsi gani, rafiki, unapooni yale Mungu atakayofanya!

⁵² Ndipo nikasimama, nikasema, “Baba wa Mbinguni, Wewe Ndiwe uliyenituma hapa, nimekuja katika Jina la Mwanao. Na nguvu hizi za pepo zimevuta hema hili...wingu hili hapa ambalo linalitikisa hema hili sana.” Ilitengenezwa tu kutokana na mbili kwa nne, lilikuwa mbali tu kadiri...Tuliwaingiza karibu elfu thelathini chini yake. Nami nikasema, “Angalia tu

kinachotendeka.” Nikasema, “Ninaikemea hiyo dhoruba basi, kulingana na ono sasa hivi, katika Jina la Bwana Yesu.”

⁵³ Nayo ikarudi nyuma ikitengana namna *hii*, jua likaangaza kwa utulivu likipenya kupitia kwake. Maelfu, mara maelfu ya Wakomunisti wakakimbia kuzunguka madhabahu, wakiitoa mioyo yao kwa Bwana Yesu Kristo.

⁵⁴ Msichana mdogo, sikuwa nimewahi kumwona maishani mwake, akisimama pale, alifumbuliwa macho katika dakika chache tu. Mama yake akaruka kwa nguvu sana huko nyuma, akatupa kiatu kimoja upande mmoja na kimoja mwingine, kisha akakimbia jukwaani kumshikilia msichana wake mdogo, aliyekuwa amezaliwa kipofu.

⁵⁵ Naye akarusha-rusha mikono yake kote, bila shaka nisingeweza kuelewa, ilikuwa katika Kijerumani, akisema, “Mama! Mama! Huyu ni wewe, Mama? Loo, wewe ni mrembo sana!” Mara ya kwanza alipowahi kumwona mama yake.

⁵⁶ Na, loo, Yeye angali ni Yehova Mungu. Yesu Kristo angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Usiogope, kaa tu kimya, mtumainie Mungu, amini kwa moyo wako wote, kuwa na hakika na hatua yako, kisha usonge mbele na Mungu. Omba, na umpende. Upendo ndio nguvu yenye uweza mkubwa kuliko zote zilizopo ulimwenguni, hakuna kitu kikuu kama upendo, nguvu ziko tu katika upendo. Tutaingilia mambo haya baadaye katika juma hili.

⁵⁷ Vema, nimekuwa nikizungumza sana. Je, lingekuwa jambo gumu sana kuwauliza tena kwa dakika chache tu, kama ningewaomba mwinamishe vichwa vyenu tunapomwomba Bwana atusaidie sasa katika somo lijalo?

⁵⁸ Baba Mungu, ninapoanza kuzungumza wakati fulani kote ulimwenguni, jinsi nilivyokuona katika vita vikuu, na jinsi Wewe ulivyo Mungu wa vita, kama vile Wewe ulivyo Mungu wa upendo. Wewe ni Yehova mkuu, mwenyezi, atoshelezaye kwa yote, wa Milele. Kabla hapajakuwapo na ulimwengu, kabla hapajakuwapo na atomi, ama molekuli Wewe ulikuwa Mungu, na wakati hakuna tena molekuli au atomi Wewe bado utakuwa Mungu. Wewe ni tangu milele hata milele, Wewe ni Mungu.

⁵⁹ Sasa usiku wa leo, tuna...Inaonekana kama, nikihisi moyoni mwangu, kwamba ningesoma sehemu kubwa ya Maandiko Yako. Nami naomba ya kwamba utanisaidia na kumtuma Roho Mtakatifu na kufasiri Neno, kusudi liweze kuleta msingi imara wa Mungu wa Milele. Na juu ya msingi wa kumpokea Yeye, ili tuweze kujiweka tayari mahali petu kwa ajili ya mkutano mkuu ambao tunatarajia kuanzisha hapa, kwamba hautakwisha mpaka Yesu atakapokuja.

⁶⁰ Bariiki kila dhehebu humu bondeni, watu wote waliobarikiwa, wahudumu na wachungaji wa madhehebu mbalimbali. Labda huenda tusikubaliane juu ya baadhi ya

mafundisho ya kitheolojia ya Maandiko, lakini Baba, yote katika kanuni moja, tunamwamini Mungu, Yule wa Milele. Kwa hiyo tusaaidie, Bwana, tuwe na umoja wa roho, mpaka umoja wa imani utakapoletwa. Na tutakapomwona uso kwa uso, ndipo tutaonana jicho kwa jicho. Mpaka wakati huo, Roho Mtakatifu na atubariki katika jitihada zetu tunazofanya. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁶¹ Katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, ama, Yohana wa Kwanza 1:7, tunasoma maneno haya:

Lakini tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo, Mwanawe, yatusafisha dhambi yote.

⁶² Yohana wa Kwanza 1:7, ninyi mnaoyaandika Maandiko. Na kama mkifanya hivyo, ningewatakeni, mtakapoenda nyumbani usiku wa leo, kwa ajili ya msingi, kupata msingi wa hili, mngesoma Kitabu cha Waebrania mlango wote wa 9, ukionyesha msingi wa damu ya mafahali, na kadhalika, na ya kondoo, msingi wa mawazo yangu. Halafu pia, Hesabu mlango wa 19, kama mnaliandika, Hesabu 19.

⁶³ Sasa, ninatoa kutoka kwenye fungu hili, mawazo haya: *Ninii . . . Njia Iliyowekwa Na Mungu Ya Kuuendea Ushirika. Njia Iliyowekwa Na Mungu Ya Kuuendea . . . Kuuendea Ushirika.*

⁶⁴ Niliwazia jambo hili asubuhi ya leo tulipokuwa na ule wakati kwenye kiamshakinywa. Tulikuwa na wakati wa ajabu sana, mzuri sana, ninii, tukikutana na wahudumu mbalimbali, wake zao, marafiki, tukipeana mikono, nikaanza kuwazia juu ya wazo hili la ushirika. Ni kitu gani kinachowafanya watu watake kufanya ushirika? Kinasababishwa na nini? Kwa nini watu wanapenda kukusanyika pamoja?

⁶⁵ Kama hapa usiku wa leo tukiketi katika jengo hili lenye joto, kidogo kuna joto sana, hata hivyo nimewaona wakiketi juu ya ngozi za wanyama katika maeneo yaliyoganda ya kaskazini, mpaka ningesimama huku nimevaa skafu kubwa ya manyoya shingoni mwangu, nimevaa kofia kubwa, pumzi ikiganda wakati ningehubiri, nao wangekaa saa baada ya saa, wakiwaweka watoto wao wadogo, Wahindi, vifuani mwao na kuwashika. Niliwaona wameketi kwenye mchanga unaowaka moto wa majangwa, mpaka, ilionekana kana kwamba, wangeungua, na bado washikilie.

⁶⁶ Kushirikiana katika Neno, kuna jambo fulani kuu kulihusu. Mwanadamu anapenda kufanya ushirika, hata kwa mtu asiyeongoka, atataka mkataba wa biashara, atatoka aende kuzungumza na rafiki yake, anunue chakula kidogo cha jioni. Nao wataketi pamoja na kula, wazungumze juu ya shida za biashara, na kufanya ushirika wao kwa wao, kwa sababu wana mambo shirika. Kama vile maskini mama yangu wa kusini

alivyozea kuniambia, “Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba.” Huo ni ukweli mwingi katika huo.

⁶⁷ Nami nashangaa kuhusu hilo basi kama tutarudi kwenye mwanzo, mambo yote yalianzia katika Mwanzo. Na katika Mwanzo, tunaona ya kwamba Mungu alimwumba mwanadamu kwa ajili ya ushirika Wake. Mungu alipenda kushuka na kufanya ushirika pamoja na watu Wake. Mungu, hapo mwanzo, Mwanzo 1: “Hapo mwanzo, Mungu,” neno hilo hapo katika Kiebrania ni *El, Elah, Elohimu*, “Yeye ajitoshelezaye kwa yote, Yeye aishiye peke yake, Mwenye nguvu.”

⁶⁸ Na ndani Yake mlikuwamo na sifa za kuwa Baba, ndani Yake mlikuwamo sifa za kuwa Mwana, ndani Yake mlikuwamo sifa za kuwa Mwokozi, ndani Yake mlikuwamo na sifa za kuwa Mponyaji, ndani Yake mlikuwamo na sifa za kuwa Mungu. Hakukuwa na kitu ila Mungu, na Mungu peke yake. Sasa, sifa hizi zilikuwa ndani Yake, basi hiyo ilizifanya kudhihirisha kitu kumwabudu Yeye. Kitu cha kwanza alichofanya kilikuwa ni viumbe vya kimalaika, nao wakamwabudu, wasingeweza kuanguka. Ndipo akamweka mwanadamu katika mwili, akaanguka kwa uhuru wa kujichagulia, alipewa haki ya kuchagua mema na mabaya.

⁶⁹ Lakini Mungu, hapo mwanzo, nadhani ulikuwa ni wakati mzuri sana, wakati Mungu wetu wa thamani, mwenye neema, aliposhuka katika bustani ya Edeni wakati wa machweo, naye angezungumza na Adamu na Hawa, nao wangefanya ushirika.

⁷⁰ Loo, ninaweza tu kuwaona Adamu na Hawa wakishuka kupitia bustanini, huku upepo ukivuma, Hawa, maskini bibi-arusi, akisema, “Loo, Adamu, u—upepo unavuma kwa nguvu sana.”

Angesema, “Amani.”

⁷¹ Mnaona, mwanadamu kwa kweli alifanywa kuwa mungu. Mnajua hilo? Biblia, Yesu alisema, “Kama waliwaita wale waliojiliwa na Neno la Mungu,” ambao walikuwa ni manabii, “kama walikuwa miungu basi mnawezaje kunihukumu Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?”

⁷² Manabii walihesabiwa kuwa miungu. Mwanadamu alipewa. . . akafanywa mungu mdogo, na kupewa milki duniani. Hiyo ndiyo sababu ulimwengu leo hii unaugua, ukingojea madhihirisho kamili ya wana wa Mungu. Loo, kuna mafundisho makuu, ya kilindi, na yenye baraka katika hilo, kwamba siku moja mwanadamu bado ataparudia mahali pake panapofaa, na milki yake itakuwa hii dunia, naye atasema na mti, au na mlima, au na chochote, nacho kitaenda tu mahali pake, kama tu ilivyokusudiwa kuwa. Sisi ni viumbe vilivyoanguka.

⁷³ Ndipo mara tu ushirika huu mkuu ambao Mungu alikuwa nao pamoja na watoto Wake katika bustani ya Edeni, wakati Malaika au mtu fulani hapana shaka alileta ujumbe, na kusema,

“Watoto wako wameanguka, nao wametenda dhambi,” basi ninaweza kumwona Mungu akija kwenye bustani Mwenyewe.

⁷⁴ Mliona? Yeye kamwe hakumtuma Malaika, kamwe hakumtuma mtumishi fulani, Yeye alikuja Mwenyewe. Ndipo akaenda huku na huko bustanini, akipaza sauti, “Adamu, Adamu, uko wapi?”

⁷⁵ Loo, ni mfano wa jinsi gani tungeweza kutoa hapo! Katika ulimwengu huu siku hizi wakati watu wenye injili ya kijamii wanapojaribu kumfanya Yesu Kristo nabii tu... Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii, Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Mungu kamwe hakumtuma nabii wala Malaika, Yeye aliumba mwili katika tumbo la uzazi la bikira Mariamu, Naye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mungu aliyaacha maeneo Yake Mwenyewe ya Utukufu, Naye akavuka tabaka Lake Mwenyewe ashuke na kuwa mwanadamu apate kuishi miongoni mwetu.

⁷⁶ Ningetaka kuzungumza juu ya hilo usiku fulani: *Ishara Kuu*, jinsi ambavyo alitandaza hema Lake hapa chini kukaa na kuwa mwa—mwanadamu, tupate kujua tabia ya Mungu. Tunapomwona Yesu, tunamwona Mungu ndani Yake, tunaona kile Mungu alichokuwa, na asili ya Mungu. Alidhihirisha, alionyesha kile Mungu alichokuwa, kumkomboa mwanadamu arudi kwa nafsi Yake tena.

⁷⁷ Na jinsi ambavyo hapo mwanzoni, wakati mwanadamu alipopotea, Mungu kamwe hakumtuma Malaika, Yeye alikuja Mwenyewe na akatafuta. Naye akatafuta kupitia bustanini, na chini ya kila kichaka, na nyuma ya kila mti, mpaka akawapata watoto Wake waliopotea. Ndipo alipowapata, ushirika Wake ulivunjika. Wasingeweza kuabudu, wakatoka mbele Zake, kwa sababu walikuwa wamejitengenezea kifuniko, bali hakingefaa kitu.

⁷⁸ Hivi mliona? Mara mwanadamu anapoanguka... anapoona kwamba ameanguka, naye asili yake ni mwenye dhambi, yeye hujaribu kujitengenezea njia ya kumwendea Mungu, ajifanyie mwenyewe dini, “Vema, simdhuru mtu yeyote. Nami ninajisikia mimi ni mzuri tu kama huyo mtu mwingine, ninatekeleza Kanuni Kuu.”

⁷⁹ Huo haukuwa mpango wa Mungu. Ili kurejesha ushirika tena, Mungu alituandalia njia papo hapo bustanini. Kama kungekuwako na uandalizi mwingine wowote ulio bora zaidi, Mungu angaliuandaa. Lakini Mungu alifanya maandalizi ya pekee, na msingi pekee wa kurejeshwa kwa huo ushirika wa Milele uliobarikiwa, hiyo ilikuwa ni kwa damu ya mwathiriwa asiye na hatia; Mungu alifanya njia ya kurejea kwenye ushirika.

⁸⁰ Huo ndio msingi pekee ambao Mungu amewahi kuwa nao, ama alio nao sasa, ama atakaowahi kuwa nao. Kurejea kwenye uhusiano na ushirika na Mungu ni kupitia kwa damu iliyomwagika ya mwathiriwa asiye na hatia. Amina. Inanifanya

nijisikie kubarikiwa, nikijua ya kwamba kuna njia, kwamba kuna njia iliyowekwa na Mungu.

⁸¹ Na ni kitu gani kilichomfanya Mungu kuiandaa njia hii? Kwa sababu Mungu ni upendo, nao upendo hudai ushirika. Upendo hudai ushirika, kama vile mvulana mdogo anapokutana na—na msichana. Na loo, ana macho kama almasi, na ana meno kama lulu, na shingo kama bata maji, na loo, yeye ndiye kitu kirembo kuliko vyote ulimwenguni.

⁸² Sasa, kamwe huwezi kupanda juu, na kusema, “Wewe ni wangu, haya twende,” hapana budi pawe na namna fulani ya mapatano. Makubaliano ya namna fulani hayana budi kufikiwa, kabla hujaweza kuingia katika ushirika pamoja na msichana huyu, inakubidi kufikia mapatano. Na hiyo ndiyo njia tunapomwona Mungu, na kujua ya kwamba Yeye ni Mungu. Tunaangalia uumbaji Wake, na Utu Wake mkuu, yale amefanya na jinsi Yeye alivyo mkuu. Ndipo inabidi . . . hatuna budi kuja juu ya msingi wa mapatano ya Mungu, hiyo ilikuwa ni kwa njia ya Damu, hiyo ndiyo njia pekee.

⁸³ Hatutaweza kamwe kuwaelimisha wampate Kristo. Jamii leo hii, na karibu zote tunazoita jamii, zimezaa wahalifu wengi zaidi ya wale waliozaliwa na wa—wahuni wote wa duniani. Watu wenye nia nyingi zaidi za uhalifu hutoka kwenye kile kinachojulikana kama jamii bora, kulingana na rekodi za FBI. Sasa, na kisha ati kuwaelimisha? Wanakuwa werevu sana hata wanafikiri wanaweza kushinda sheria, wanajua zaidi ya mtu mwingine.

⁸⁴ Elimu ni nzuri sana. Ndilo jambo . . . Sijaribu kuunga mkono ujinga, bali ninajaribu kusema hivi: Kwamba elimu imeninii, imekuwa ni moja ya kizuizi kikuu sana ambacho dini ya Kristo imewahi kuwa nacho. Watu wanachukua na kutumia shule zao za theolojia kujaribu kuwaelimisha watu kwa kuzungumza vizuri, na jinsi ya kujiwasilisha, na kadhalika, nao wanaenda moja kwa moja mbali na Roho. Mungu hajulikani kwa elimu, Mungu hajulikani kwa madhehebu, Mungu hajulikani kwa kanuni za imani. Mungu anajulikana kwa imani na hiyo pekee. Ni kwa imani tunaokolewa. Mungu anajulikana kwa imani.

⁸⁵ Sasa, hata katika madhehebu yetu, kadiri yalivyo mazuri, na kadiri tunavyopaswa kuyahifadhi, na—na kuyaheshimu, hata hivyo hakuna dhehebu linaloweza kumwokoza mtu, hakuna dhehebu linaloweza kukuingiza katika ushirika, isipokuwa uje kwa Damu. Huna budi kuja, si kwa kanuni yako ya imani, bali kwa Damu.

⁸⁶ Na kanuni za imani, na kujiunga na makanisa, na madhehebu kamwe hayataridhisha moyo wenye njaa, kuna kitu kimoja tu kinachoweza kutuliza kiu cha moyo wenye kiu, hapo ni wakati anapotakaswa kwa Damu ya Bwana Yesu Kristo, na Roho

Mtakatifu anaingia katika ushirika pamoja naye, kumrudisha katika uhusiano na ushirika.

⁸⁷ Mungu daima amekuwa na njia ya Damu kuwatakasa watu Wake, na kuwaleta mahali pa ushirika pamoja Naye tena. Sasa, katika Agano la Kale katika Hesabu 19 walipokuwa katika safari yao, Mungu alimwita Musa na Haruni na kusema, “Waagize wana wa Israeli kwamba wewe... wakuletee ndama mwekundu, ndama mwekundu asiye na ila wala waa.”

⁸⁸ Mfano mzuri wa Kristo tena, nyekundu ikiwa ni ishara mbaya, ishara ya hatari, hata hivyo ni ishara ya ukombozi. Mchirizi wa damu umekuwa wote, ni uzi kote kote katika Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo.

⁸⁹ “Nileteeni ndama mwekundu ambaye hajatiwa nira juu yake kamwe.” Hajatiwa nira na kitu kingine chochote. “Mleteni, na aletwe mbele ya Eleazari, Kuhani Mkuu, na kusanyiko, nao wamwue. Naye Eleazari atie vidole vyake katika hiyo damu na kunyunyizia mara saba juu ya mlango wa kusanyiko.” Kisha kasema, “Nao wauteketeze mwili wake pamoja na kwato zake, pamoja na pembe zake, na yote aliyo nayo. Kisha watwae sufu nyekundu, na hisopo, na mti wa mwerezi, na kuvitupa katika hiyo dhabihu, na kuvitekeza pamoja.”

⁹⁰ Ndipo basi walipaswa kuvichanganya na maji, na kuviweka kwenye, mahali safi. Nayo yalikuwa yawe maji ya farakano, kumtenganisha mwenye dhambi, Mkristo, na dhambi zake, kumleta katika ushirika tena. Sasa, ni jambo gani lililotukia? Kama msafiri, ama mgeni, ama au wana wa Israeli walikuwa wametenda dhambi na kutenda mabaya, walifika kwenye nyua za nje kwanza.

⁹¹ Nami ninawatakeni mwone kule kuchanganyisha dhabihu, vizuri. Sasa, ya kwanza, mierezi ilitiwa ndani, sufu nyekundu, na hisopo. Hizo elementi tatu, mnaona zinatumiwa katika Biblia mara nyingi, zinazungumza juu ya agano. Sasa, hebu chukua kipande cha kioo chenye pembe tatu na kukiangazia nuru, jua, kitatoa hizi saba mbalimbali, rangi ya upinde wa mvua. Kama utaweka rangi tatu na dhidi ya jua, zitaonyesha upinde wa mvua, nao upinde wa mvua unawakilisha agano.

⁹² Sasa, nilijifunza jambo hili muda fulani uliopita kuhusu ni nini maana ya rangi nyekundu katika Biblia? Nyekundu ilikuwa sufu ya kondoo dume iliyokuwa imetiwa damu, wakijua ya kwamba kitu fulani kilikufa ili kumpaka mnyama rangi tofauti. Huyu kondoo dume alikuwa na rangi ya kijivu, kijivu, ambayo ni rangi ya kinafiki. Lakini mara alipopakwa rangi nyekundu! Na mtu yeyote hapa anayejua lolote kuhusu sayansi, anajua ya kwamba unaweza kuchukua kitu chochote chekundu na kuangalia nyekundu, na nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe.

⁹³ Kwa hiyo, dhambi zako zikiwa nyekundu sana, na Mungu aziangalie kupitia Damu ya Mwanawe, unakuwa mweupe kama theluji. Nyekundu ikipitishiwa nyekundu inaonekana nyeupe, hiyo ndiyo njia ya kukaribia; nyekundu ikiangaliwa kwa nyekundu inageuka nyeupe. Mungu, akimwangalia mwenye dhambi, ambaye amekiri yeye ni mwenye dhambi na amekubali njia iliyowekwa na Mungu ya kumwendea, Mungu anamwona mweupe kama theluji, haya basi, kuangalia nyekundu kupitia nyekundu.

⁹⁴ Hawezi kuangalia kupitia kanuni ya imani, hawezi kuangalia kupitia madhehebu, hawezi kuangalia kupitia kitu kingine. Lazima iwe ni Damu na Damu pekee. Loo, ninakumbuka ule wimbo wa kale wa Jeshi la Wokovu:

Loo, mtiririko huo ni wa thamani,
Ambao hunifanya mweupe kama theluji;
Sijui chemchemi nyingine,
Hakuna chochote ila Damu Yake Yesu.

⁹⁵ Loo, hizo nyimbo za kale! Kuimba juu ya Damu, kungemleta Roho wa Mungu miongoni mwa kusanyiko. Ninakumbuka huko chini Kentucky, kanisa la kale la Kimishenari la Kibaptisti, wakati tulipozoea kuimba, “Nimepita pazia lililopasuliwa, Ee utukufu kwa Jina Lake. Niko ng’ambo ya pili, Haleluya kwa Mwana-kondoo,” nguvu za Mungu zingeshuka katika maskini kusanyiko hilo dogo kando ya mlima pale, wangepiga makelele na kupiga mayowe, na kutembea huku na huko kwenye marefu ya kanisa, wakipeperusha mikono yao.

⁹⁶ Loo, walikuwa Wabaptisti halisi, si kama baadhi ya Wabaptisti hapa, ati njoo huku na kupeana mikono, na kuandika jina lako kwenye karatasi. Tulishuka, tukapigana mgongoni mmoja na mwenzake mpaka tukapita, tulikuwa na kitu fulani. Hao ni Wabaptisti halisi, ambao kweli wanakaa pale mpaka jambo fulani litukie, wakiimba zile nyimbo za kale za Damu.

⁹⁷ Sasa, basi tena, sufu ya kondoo dume iliyotiwa damu ilikuwa nyekundu. Hisopo ni gugu la kawaida tu, inapatikana Misri, na inapatikana Palestina, kwa kawaida inakulia kwenye nyufa za jengo. Ni kitu kama kichaka kidogo, kina ua dogo jeupe juu yake, cha kawaida tu, kinaweza kupatikana popote. Hiyo ilinena juu ya nini? Imani, hisopo, imani, ni ya kawaida tu. Unafikiri inakubidi kuwa na imani fulani ya kimbinguni kupata kitu kutoka kwa Mungu, sivyo, imani ya kawaida tu kama uliyo nayo, tia tu Damu.

⁹⁸ Mnakumbuka usiku wa Pasaka, walichukua hi—hisopo na kuinyunyizia vizingiti vya mlango na mwimo kwa damu, ulionyunyiziwa damu kwa hisopo? Imani rahisi, kama ya kitoto.

⁹⁹ Kama umeketi hapa sasa wala hujawahi kukutana na Yesu maishani mwako, tumia tu hiyo imani ndogo, rahisi iliyokuleta kwenye jengo hili usiku wa leo. Haikubidi kwenda shuleni na

kujua theolojia fulani kuu, ama—ama kukariri kanuni fulani kuu, ndefu za imani, na kutaja majina ambayo yule anayekupa hajui maana yake. Jambo pekee unalopaswa kujua ni kujua ya kwamba Yesu alikufa ili kuwaokoa wenye dhambi, nayo Damu Yake inakuosha ukawa mweupe kama theluji. Jambo ndilo hilo, imani rahisi kama ya kitoto.

¹⁰⁰ Kama wewe ni mgonjwa, unaona kazi ya Roho Mtakatifu, usifikiri inakubidi, “Loo, Ndugu Jones, niombe nipate imani zaidi.” Umeipata. Chukua tu gugu rahisi la hisopo, linalopatikana tu mahali popote, na upake Damu. Loo, Mungu, jambo ndilo hilo! Si kitu fulani cha kishirikina ama baadhi ya mambo ya kipumbavu unayopitia, hayo siyo. Ni imani rahisi tu ya kitoto kupaka Damu. Amini kwa moyo wako wote, litatukia.

¹⁰¹ Na kisha mti wa mwerezi, mwerezi ni mwekundu au mweupe. Sote tunajua ya kwamba nyekundu kupitia nyekundu hufanya nyeupe. Na sufu nyekundu sana, hisopo, mti wa mwerezi uliowekwa pamoja na ndama mwekundu, na kuchomwa pamoja, vikichanganywa na maji, hayo yalikuwa ni maji pamoja na majivu. Sasa, maji hunena juu ya Roho, majivu hunena juu ya Neno. Ndipo Neno na Roho wanapokutana, jambo fulani hutukia.

¹⁰² Wakati Roho wa kweli wa Mungu anapoweza kuingia juu ya Neno linalohubiriwa, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno,” naye Roho wa kweli wa Mungu anapolishika Neno hilo, atadhihirisha kila ahadi ambayo Mungu alitoa, ataitimiza na kuifanya itendeke. Mtazamo mzuri wa kiakili kwa ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu utaifanya kutimia, kama ungeweza kumpata Roho pamoja na Neno.

¹⁰³ Mnakumbuka ile hadithi jana usiku, yule mwanamke kisimani? Yesu alimwambia, kama ukiisoma leo katika Yohana Mtakatifu 4, “Baba anawatafuta watu kama hao watakaomwabudu katika Roho na katika Kweli.” Nalo Neno Lake ni Kweli. “Roho na Kweli.”

¹⁰⁴ Watu wengi wana Roho bila Kweli, wengine wana Kweli bila Roho. Ni kama mtu aliye na pesa kwenye benki, wala hajui kuandika hundi, huyo mwingine anajua kuandika hundi, wala hana pesa kwenye benki. Laiti ungaliweza kuwaleta hao wawili pamoja! Roho na Kweli, Neno lililo na Roho ndani Yake.

¹⁰⁵ Nimepata mengi sana ya hayo katika wakati wangu, baadhi ya watu walikuwa na roho kwelikweli, bali hawakuwa na kweli. Kwenu mliokuwa kwenye kiamshakinywa asubuhi ya leo, lile somo nililozungumzia, nina hakika mnaelewa ninalomaanisha. Vema, mna kweli, imewekwa katika utaratibu, kanisa pamoja na Neno, basi acha Roho ashuke aingie pamoja na Neno, na kisha uangalie yatakayotukia, yatajidhihirisha kila wakati.

¹⁰⁶ Sasa, asiyeamini akiingia, jambo la kwanza alilofanya, ilimbidi kufanya hivyo kama tu ninii... alikuja kwenye maji

haya ya farakano kwanza, apate kutenganishwa. Sasa, anakuja nini? “Imani chanzo chake ni kusikia.” Alikuwa kwenye ua wa nje. Sasa, lazima iwekwe mahali safi.

¹⁰⁷ Nalo Neno la Mungu linapaswa kuwekwa mahali safi. Moyo mchafu hauna nafasi kwa ajili ya Neno la Mungu, Linapaswa kuwekwa katika moyo wa kweli, usioghoishiwa, ambao umetengwa na mambo ya ulimwengu. “Ukiipenda dunia, ama mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hakumo ndani yako.” Maandiko yanasema hivyo. Ndipo watu siku hizi. . .

¹⁰⁸ Kwa nini makanisa yetu hayaendi mbele jinsi yanavyopaswa kufanya, yana ulimwengu mwingi kupita kiasi mle ndani, yakijaribu kuchanganya maji ya farakano Nalo, Nalo halina budi kuwekwa mahali safi kuona madhihirisho ya Roho, katika moyo safi, lililowekwa mahali safi.

¹⁰⁹ Ndipo mwenye dhambi akaja, naye alikuwa...akakiri kwamba alikuwa ametenda dhambi na kufanya makosa, kisha akanyunyiziwa maji ya farakano.

¹¹⁰ Sasa, bila kujali dhehebu langu la Kibaptisti ambalo nilikuwa... nililipenda sana, bali niliambiwa nao ya kwamba hivyo ndivyo tulivyofanya, tulimwamini tu Mungu, ndipo tukazaliwa mara ya pili kwa Roho, lakini nikaja kugundua ya kwamba hiyo haikuwa kweli yote hasa. Mnaona, daima waliniambia ya kwamba Matendo 19 ilisema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu...? Mlimpokea Roho Mtakatifu *wakati* mlipoamini.” Lakini Biblia inasema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?” tangu mlipoamini. Sasa, hivyo ndivyo Paulo alivyouliza, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?”

¹¹¹ Hao walikuwa Wabaptisti, pia. Wangalikuwa wameongoka chini ya mafundisho ya Apolo. Alikuwa mwanasheria aliyeongoka, ambaye alikuwa amemwamini Mungu kupitia kwa Yohana Mbatizaji, nao walikuwa ni Wabatisti halisi, wakibatizwa, na wakiwa na ushirika mkuu, na kuthibitisha kwa Neno ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo. Lakini wakati Paulo alipokuja na baraka za Kipentekoste, alisema, “Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Hilo lilikuwa ndilo swali.

¹¹² Sasa, watu wengi hufikiri wanapokuja na kufanya maungamo, kukiri dhambi zao, kwamba Mungu huwanyunyizia maji ya farakano, na ni hayo tu. La, bwana. Ndio kwanza unaanza sasa, hujafika kwenye ushirika.

¹¹³ Tafadhalini samahani mafundisho haya makali sana, fidhuli, lakini mimi—mimi... Wewe... Kabla hujaweza kufanya ninii... Mtu *huyu* ni seremala, naamini alisema, ama... Kabla hujaweza kufanya ubao ushikilie vizuri kwenye nyumba, huna budi kupigilia hiyo misumari. Hiyo ni kweli? Hivyo ndivyo Injili,

inakubidi kuipigilia ndani, kuifanya ishikilie pale pamoja na Neno.

¹¹⁴ Sasa angalieni, wakati baada ya mwaminio huyu kuja na kumkubali Mungu, na upatanisho wa dhambi zake, alinyunyiziwa maji ya farakano, ilikuwa ni kutakaswa. Katika Waefeso 6:5, naamini, ama 5:6, hasa, naamini ndivyo ilivyo, unaona ya kwamba Paulo alisema, “Tumeoshwa kwa maji ya Neno,” maji ya farakano yanayotuosha. “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.” Inatutenganisha tu na dhambi zetu. Sasa, usibaki hapo, ndugu au dada yangu wa thamani, bado hujaukaribia ushirika.

¹¹⁵ Angalia, jambo lingine linalotukia, baada ya mnyama huyo kuuawa, na maji ya farakano kufanywa, ambayo yalinena juu ya Kristo, yale maji ya farakano yalitolewa, kisha baada ya huyu asiyeamini, akitengwa na dhambi zake, ndipo akaliangalia kusanyiko, kuelekea kwenye lile—lile jengo, na alipoingia mahali patakatifu ama ua la pili, ilimbidi akumbuke juu ya mlango huo kulikuwa na milia saba ya damu, kitu fulani hicho cha kumruhusu aingia katika ushirika, kilikufa na kumtangulia.

¹¹⁶ Ingawa Neno limetusafisha kwa kusikia, kwa imani, hata hivyo hatuna budi kuitambua hiyo Damu, kwamba kitu Fulani kilikufa na kututangulia kikaisafishe njia. Loo, Jina la Bwana libarikiwe! Kitu fulani kweli kilikufa kwa ajili yetu, Bwana Yesu Kristo alituachia Neno La—Lake, na hiyo hapo Damu Yake kama kumbukumbu.

¹¹⁷ Sasa, basi tunapoenda kule, baada ya kusafishwa na Neno, maji ya farakano, tunatembea kuelekea kwenye mlango wa maskani, tunasimama. Loo, laiti tungalikuwa na wakati wa kukaa hapa mlangoni kwa dakika chache, kile milia hiyo saba juu ya mlango ilichomaanisha! Nyakati saba, yale majira saba ya wakati wa kanisa. Kila wakati tangu Mwanzo hadi mwisho wa Ufunuo, imekuwa ni Damu katika kila wakati wa kanisa. Hakuna kanuni za imani, hakuna mafundisho, hakuna chochote ila Damu ya Bwana Yesu.

¹¹⁸ Bado hujaingia katika ushirika. Umetengwa na dhambi zako, ukitambua sasa kupitia utakaso, kule kutakaswa, kwamba Kitu fulani kilikufa na kikakutangulia. Lakini angalia, walitoka mahali hapo wakaingia katika Patakatifu pa patakatifu. Loo, mtu mmoja alienda mara moja kwa mwaka, Haruni, kuhani mkuu, akienda na damu mbele yake. Angalieni, alikuwa amevalia kwa njia fulani, mfano mzuri wa Kanisa, kama mtalipokea.

¹¹⁹ Sasa kumbukeni, ungeweza kushiriki pamoja na kusanyiko mara tu uliponyunyiziwa majivu, kwa sababu ungeingizwa kama mwaminio. Unapofika uani, ungeweza kufanya ushirika pamoja nao mle ndani, hiyo ni kweli.

¹²⁰ Na leo, kama vile katika kanisa la Kibaptisti, haidhuru umebatizwa katika kanisa gani, unapokuja kwenye kanisa la Kibaptisti, huna budi kubatizwa tena, kwa sababu unabatizwa katika ushirika wa Kibaptisti, ninyi Wabaptisti wote mnajua hilo. Mkristo, kanisa la Kikristo hubatiza kwa kuzamisha, haidhuru alikubatiza kiasi gani, hatuna budi kukubatiza tena, maana unabatizwa katika ushirika wa imani ya Kibaptisti. Ni mfano wa jinsi gani, ni onyesho la jinsi gani hapa!

¹²¹ Angalia, unapokuja katika farakano, ukifanya maungamo, vema, unaweza kufanya ushirika nao. Unaingia basi chini ya Damu, unaweza kufanya ushirika nao chini ya Damu, hiyo ni kweli vya kutosha. Lakini kufanya ushirika na Mungu, inakubidi kwenda Mbele za Mungu, na hiyo ni katika Utukufu wa Shekina.

¹²² Na mtu mmoja mara moja kwa mwaka alikuwa amevalishwa nguo apate kuingia katika Utukufu wa Shekina, ambamo alifanya ushirika na Mungu uso kwa uso. Mbona, kulikuwa na utukufu sana mle ndani, mwaka mmoja aliacha fimbo yake, nayo ikachanua na kuchanua katika Uwepo wa Utukufu wa Shekina.

¹²³ Ndugu, dada, leo hii, unasema, “Lakini Ndugu Branham, mara moja kwa mwaka?”

¹²⁴ Naam. Angalia jinsi ilivyombidi kuvalishwa: ilibidi avae vazi fulani lililotengenezwa kwa mikono fulani, mikono mitakatifu. Ilimbidi kutembea hivi kwamba, kwenye vazi lake alikuwa na komamanga na kengele, na kila wakati aliposogeza miguu yake, akisogea namna hiyo, ilicheza, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana.” Anafanya nini? Anaukaribia Utukufu wa Shekina kwa ajili ya ushirika pamoja na Mungu Mwenyewe, akiibeba ile damu mbele zake. Ee Mungu, laiti ningalikuwa na sauti ya Malaika, ningeweza kufanya hilo lizame ndani.

¹²⁵ Hakutoka akaenda akisema, “Mimi ni Mpresbiteri.” “Mimi ni Mmethodisti.” “Mimi ni Mpentekoste.” Loo, ilikuwa ikicheza, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu...” Akiwa amebeba damu, damu ilimtangulia, akitambua mwathiriwa asiye na hatia alikufa.

¹²⁶ Basi kumbukeni, alitiwa mafuta ya thamani ya kupaka, hata Biblia ilisema, “Jinsi ilivyo vema ndugu wakae pamoja, kwa umoja! Ni kama mafuta ya kupaka yaliyokuwa kichwani mwa Haruni, yashukayo hata upindo wa mavazi yake.” Alikuwa amefunikwa kabisa na harufu nzuri ya Bwana.

¹²⁷ Loo, ni mavazi ya jinsi gani! Jinsi Mungu angetaka kuliweka Kanisa Lake katika hali hiyo! Njoni kwenye maji ya farakano, ungameni dhambi zenu. Vema, hilo ni zuri. Halafu, tunatembea na kutakaswa na mambo yote ya ulimwengu, kama vile Damu inavyotutakasa.

¹²⁸ Waebrania 13:12 na 13 ilisema, “Yesu aliteswa nje ya malango ili awatakase watu kwa Damu Yake Mwenyewe.” Basi bado usisimame, hujaja bado, chukua Damu hiyo moyoni mwako, ingia ukiwa na upako wa Roho juu yako, loo, jamani, wakibeba ile Damu, wakitembea, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana.”

¹²⁹ Mnajua, kama hakupiga kelele hizo nyuma ya pazia hilo, watu hawakujua kama alikuwa amekufa au alikuwa hai. Hiyo ndiyo njia pekee wanguweza kujua kama alikuwa angali anaishi katika ule utukufu mkuu, ni kwa sababu wakati alipokuwa ndani, wanguweza kusikia kelele.

¹³⁰ Sijui ni kitu gani kilichotendeka kwa kanisa, jambo fulani liliunda kombo mahali fulani. Hiyo ndiyo njia pekee wanguweza kujua alikuwa hai, kwa sababu kelele fulani zinaendelea, na watu wanaogopa kelele. Ni ishara ya kwamba tungali hai, wakati wanaume na wanawake wanapoweza kuja chini ya nguvu za Mungu aliye hai, inaonyesha ya kwamba kungali kuna Roho aliye hai ndani yetu, anayepiga kelele, kelele tukufu kwa Bwana.

¹³¹ Ndani ya Patakatifu pa patakatifu, sasa, mtu mmoja mara moja kwa mwaka aliingia mle, lakini wakati Dhabihu yetu halisi, Yesu Kristo, ilipokufa pale Kalvari, Yeye alipasua lile pazia vipande viwili, akitengeneza njia kwa Damu Yake Mwenyewe kwamba yeyote atakaye anaweza kuingia katika Utukufu wa Shekina katika Uwepo wa Roho Mtakatifu, na ajazwe na nguvu za Pentekoste, kama walivyofanya baada ya lile pazia kupasuka. Wa manjano, wa kahawia, mweusi, mweupe, mwanamume, mwanamke, Mmataifa, au Myahudi, “Kila atakaye, na aje anywe katika chemchemi ya Bwana.” Walipoingia kwenye huo Utukufu wa Shekina, wametiwa mafuta na Roho Mtakatifu, ndipo wana ushirika na Mungu tena, ndipo wao ni wana na binti za Mungu.

¹³² Si ajabu tunasimama kwenye maji ya farakano na kujaribu kufanya ushirika kutoka *hapa* mpaka chini *hapa*, huwezi kufanya hivyo. Ukisimama kando ya Damu bila kuingia mahali patakatifu, ungali hauko katika ushirika. Lakini unapochukua maandalizi yote . . .

¹³³ Ni kitu gani kilichotoka katika mwili wa Yesu alipokufa? Ku—kuzaliwa kwa kawaida kuna nini? Samahani, akina dada, nanyi wasichana, nawasihi mnisamehe, lakini nataka kutoa tamshi. Mtoto mchanga anapozaliwa kwa njia ya kawaida, kitu cha kwanza ni nini? Maji. Kitu cha pili? Damu. Kitu cha tatu? Roho. Ni kitu gani kilichotoka katika mwili wa Yesu? Maji, Damu, Roho. Amina.

¹³⁴ Wakati mtoto mchanga anapozaliwa, wala kamwe halii, kamwe hasogei, ana kasoro, ni kile kinachoitwa kuzaliwa mfu, ni mfu anapozaliwa. Ni kitu gani kinachotukia? Dakitari

anamnyanyua kwa visigino na kumtikisa, na kumpigapiga kidogo, nacho kilio kinatokea, uhai unaingia.

¹³⁵ Kanisa la Kipentekoste lina shida gani usiku wa leo? Linahitaji kichapo kingine cha Injili ambapo Roho Mtakatifu... kutikiswa kwa visigino vya Injili, ili kwamba Uhai utaingia ndani yake tena, nao watapiga kelele kwa sifa za Mungu. Loo, Yeye ni wa ajabu sana.

¹³⁶ Kama yule msichana niliyekuwa nikizungumza habari zake, yule kijana mwanamume, walipokutana, wakapendana. Jambo la kwanza linalopaswa kuwepo ni mapatano, kama wataenda pamoja, ndoa kabla hawajaingia katika ushirika. Kisha anampeleka maskini bibi-arusi huyu nyumbani kwake.

¹³⁷ Sasa, unaweza tu kuishi katika nyumba ya vyumba vitatu. Mlijua hilo? Mungu aliishi katika nyumba ya vyumba vitatu, wewe unaishi katika nyumba ya vyumba vitatu, wewe—wewe unaishi katika nyumba ya vyumba vitatu. Mungu aliishi katika Kristo: Nafsi, mwili, na Roho. Unaishi: nafsi, mwili, na roho, unaishi katika nyumba yako mwenyewe hapa duniani, huenda ukawa na vyumba viwili vya kulala, huenda ukawa na vyumba vitatu vya kulia chakula, lakini ungali unaishi tu katika nyumba ya vyumba vitatu, hivyo ni jikoni, chumba cha chakula, na chumba cha kulala, jiko, sebule, na chumba cha kulala, ninamaanisha.

¹³⁸ Sasa angalieni, cha kwanza ni kipi? Kama vile maji ya farakano, cha kwanza ni nyua za kwanza, jikoni, mahali unapokuja na kula. Unakula jikoni, kisha unakuja kanisani na unakula Neno. Loo, hivi hamlipendi Neno? Kula Neno, hapo ndipo mahali pa kwanza.

¹³⁹ Halafu mahali pengine, unaingia katika na—namna fulani ya u—u—uhusiano wa namna hii, ambapo unamkumbatia mke wako. Unasimama hapo, labda sebuleni wakati anapovua utaji wake, nawe unamkumbatia, na unamwambia unampenda, na kwamba atakuwa mke mpendwa kuliko wote kote ulimwenguni, na jinsi unavyompenda na jinsi utakavyokuwa mwaminifu kwa na—nadhiri zako za ndoa, na kadhalika. Umekwisha kufanya karamu yako ndogo, karamu ya arusi, na sasa umeingia kumwambia sebuleni. Unamketisha kitini, ama kumweka pajani mwako, na kumwambia uko tayari kuingia katika ushirika halisi.

¹⁴⁰ Samahani kwa usemi huu fidhuli, lakini huo bado haujakamilika, ushirika, kamili, unaweza tu kuja kwa uhusiano. Na jinsi tu unavyoweza kushiriki kikamilifu na mke huyu kama mke wako, hajapata kuwa ushirika mkamilifu kwako, mpaka amedumu katika uhusiano, huo ni chumba cha kulala, hapo ndipo uhai mpya unapozia.

¹⁴¹ Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kanisa siku hizi. Hatuwezi kamwe kuchukua kanuni za imani na kadhalika, na kamwe

turudishe ushirika halisi, mpaka tutakapokuwa na uhusiano na Mungu, kuzaliwa wana na binti za Mungu.

Unasema, “Hiyo ni fidhuli, Mhubiri.”

Ni kweli hata hivyo, ni kweli.

¹⁴² Angalia basi, vipi kama maskini bibi-arusi atakuja na kuketi pajani mwake, lakini yeye ni mwenye haya sana, hataki kuingia chumbani, hataki kuingia katika ushirika mkamilifu na uhusiano na mumewe? Hakutakuwako na uhai tena.

¹⁴³ Sasa, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, tunadai kuwa Bibi-arusi wa Kristo, tunadai sisi ni Bibi-arusi, na kama sisi ni Bibi-arusi, tunapaswa kuwa tukizaa watoto, hatuionei haya Injili.

¹⁴⁴ Nilipotembea kwa mara ya kwanza miongoni mwa Wapentekoste, niliwasikia, na kundi nililokuwa nalo, mbona, lilikuwa—lilikuwa ni kundi kubwa sana, nitakubali hilo, lakini kuna jambo moja nililoona, hawakuona haya kwa jambo walilokuwa wakizungumzia, walikimbia huku na huko kwenye marefu ya kanisa, walikuwa na nguvu ambazo sikuona zikifanya kazi hapo kabla, kwa sababu walikuwa wameingia katika uhusiano na Mungu, na wakazaliwa mara ya pili, nao walikuwa wana na binti za Mungu. Wangesimama moja kwa moja mtaani na kupaza sauti, “Haleluya! Mungu asifiwe!” Wangetembea huku na huku mtaani kila mahali, wakipaza sauti na kumsifu Mungu, hawakuona haya.

¹⁴⁵ Lakini siku hizi, wanaume wetu, wanawake wetu wanaondokea jambo hilo, wanaondoka kwenye alama za mipaka za mtindo wa kale tulizokuwa tukipitia. Unapaswa kurudi kwenye alama hiyo ya kale ya mpaka ya Kipentekoste. Mnachohitaji hapa katika bonde hili, nilipoangalia kote leo, ni dini ya mtindo wa kale, iliyotumwa na Mungu, ya anga-bluu, inayoua dhambi, nguvu za Injili kurudi makanisani tena, kurudi kupitia Damu ya Bwana Yesu, kuingia katika ushirika kwa uhusiano, kwa kuzaliwa na Roho Mtakatifu, kuingia katika Shekina ya Kipentekoste. Amina.

¹⁴⁶ Sijarukwa na akili, najua mahali nilipo. Loo lakini, ndugu, dada, kutwaliwa katika Utukufu huo wa Shekina ambapo wewe na Mungu pekee mnasimama, mkifanya ushirika, hiyo ndiyo njia pekee ya kuendea niijuayo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴⁷ ...ya sadaka ya kuteketezwa. Alishikilia hilo kote maishani. Alipokuwa kijana, alilifanyia maandalizi. Ndipo basi alipozeeka, na wakati majaribu yake yalipokuja, na wakati ninii yake, ingawa alisingiziwa uongo, walimwambia, “Ayubu, wewe ni mtenda dhambi kisiri,” washiriki wa kanisa lake walikuja na kudai kwamba alikuwa amefanya maovu, Ayubu alidumisha ushirika wake vivyo hivyo, alijua alikuwa mwenye haki, kwa sababu alikuwa amepitia njia ya damu. Ilishikilia vizuri sana, mpaka hata akasema katika saa za majaribu yake,

“Ajaponiua, hata hivyo nitamtumainia.” Amina! Hivyo ndivyo Damu ifanyavyo, huo ndio ushirika kupitia kwa Damu.

148 Danieli... Si ajabu tunarudi nyuma kwa urahisi sana, si ajabu hatuwezi kushikilia kutoka kwenye uamsho mmoja hadi mwingine. Si ajabu Billy Graham mashuhuri alisema huko Louisville, Kentucky, ya kwamba Biblia ilikuwa ndiyo kipimo. Akasema, “Paulo alienda mahali fulani akapata mwongofu mmoja, akarudi mwaka uliofuata na mwongofu huyo, alikuwa na wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wa wajukuu wameongoka kwa yuyo huyo.” Nilikuwa kwenye kiamshakinywa chake huko Louisville. Naye akasema, “Nifanye nini? Ninaenda kwenye mji fulani, nami nina... ninadai waongofu elfu thelathini katika majuma sita, ninarudi katika mwaka mmoja wala siwezi kupata thelathini.”

149 Sasa, huyo mwinjilisti mkuu alikuwa na jambo zuri, lakini nafikiri aliliendea vibaya, akasema, “Jambo ni kwamba, ni ninyi wahubiri wavivu, mnaketi huku mmewekelea miguu yenu kwenye dawati wala hamtoki kwenda kuwazungumzia hao watu.” Kasema, “Jambo ndilo hilo.”

150 Nikawazia, “Lakini Billy, ni mhubiri gani aliyewekelea mguu wake dawatini pamoja na huyo mwongofu mmoja wa Paulo?” Ilikuwa ni kwa sababu kwamba, siku hizi, tunasimamia tu kwenye maji ya farakano wala hatuwaingizi katika ushirika pamoja na Roho Mtakatifu na nguvu za Utukufu wa Shekina.

151 Ukimweka mtu huyo katika hali hiyo, atauteketeza mji kwa Injili, hakuna kitu kinachoweza kumzuia. Yeye ana Roho wa Mungu juu yake, hahitaji mtu yeyote kumshawishi, Mungu yuko mumo humo ndani yake, akiiteketeza tu dhambi anapoenda. Hawezi kusimama kimya. Kwa nini? Ameingia katika ushirika kwa uhusiano.

152 Uhusiano, yeye amezaliwa mara ya pili, yeye ni kiumbe kipya katika Kristo, alipitia kwenye maji ya farakano, alitembea kupitia Damu ya utakaso, aliingia katika ushirika wa Roho Mtakatifu. Naam, bwana, akazaliwa, naye... katika ushirika, Njia pekee iliyowekwa na Mungu ya kumwendea. Hakuna njia nyingine mahali popote, hakuna wakati, wala njia yoyote, ni kupitia tu hivyo.

153 Kama nilivyosema, madhehebu yetu, ninayathamini, kanuni zetu za imani, hizo ni sawa kabisa, zinatimiza kusudi lao, lakini ndugu, kamwe hazitapachukua mahali pa Damu ya Yesu Kristo. Haziwezi, kwa sababu huo ndio msingi pekee wa Mungu. Tunapaswa kuwa na bidii kwa dhehebu letu, tukijaribu kulifanya likue, hilo ni sawa, hilo ni zuri, ninalithamini, bali hilo kamwe halitachukua mahali pa Damu. La, bwana.

154 Mwangelie Danieli chini ya dhabihu ya damu, kabla hajaondoka Yerusalemu, alikusudia moyoni mwake kwamba

hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme. Basi wakati alipotupwa kwenye tundu la simba, akahukumiwa na serikali ya shirikisho na kutupwa katika tundu la simba, alidumisha ushirika wake katika tundu la simba. Haleluya!

¹⁵⁵ Mtaniita mtakatifu anayejibingirisha, kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali tu muanze. Loo, ndugu, Damu tu ndiyo yote nijuayo, si kitu ila Damu ya Yesu.

¹⁵⁶ Danieli mbele ya simba alidumisha ushirika wake, Roho Mtakatifu akaingia moja kwa moja, akaishi huko chini pamoja naye, akazungumza naye usiku kucha.

¹⁵⁷ Wana wa Kiebrania katika tanuru ya moto, moto mkali ambao hata uliwaua watu waliowatupa ndani, wakiwa katika joto lake la tanuru, ukawaua watu waliowatupa ndani, bali walidumisha ushirika wao.

¹⁵⁸ Ibilisi hawezi kuweka majaribu juu yako kupita kiasi, pasipo wewe kudumisha ushirika huo kama umekuja kwa njia iliyowekwa na Mungu ya kuendea, wewe ni mwana wa Mungu, ulimwengu umechomwa ukatolewa kwako, umeingia katika Utukufu wa Shekina, Roho wa Mungu yuko moyoni mwako.

¹⁵⁹ Kama vile maskini Stefano, hapo walipomtupa huko nje mtaani, wakaokota hayo mawe makubwa, naye alikuwa amewahubiria nguvu za Roho Mtakatifu, akasema, na mwishowe, akasema, “Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu, kama baba zenu walivyofanya, na ninyi vivyo hivyo.”

¹⁶⁰ Loo, jamani! Whiu! Kasema uso wake uliangaza kama Malaika. Siamini uliangaza kama moja ya nuru hizo, uso wa Malaika usingeangaza namna hiyo, Malaika ni mjumbe. Lakini ni kitu gani kilichoufanya uangaze? Alijua alichokuwa akizungumzia. Malaika anajua anachozungumzia, na mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu anajua anachozungumzia, kama amewahi kuingia katika Utukufu wa Shekina. Amina.

¹⁶¹ Hilo lisikuogopeshe, *amina* linamaanisha, “Na iwe hivyo.” Hilo ndilo tu ninaloamini. *Haleluya* maana yake ni “Mungu wetu asifiwe,” Naye anastahili sifa zote. Naam!

¹⁶² Akaingia Mle, ndipo walipomchukua, wakamvuta kutoka kwenye...kutoka kwenye—kwenye Baraza la Wazee, wakamtupa nje mtaani, watu wa kanisa walimtupa, walimtupa huko nje mtaani, kwa sababu alikuwa na ushirika kwa njia ya uhusiano kwa Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Wakaokota mawe na kuanza kukiponda-ponda kichwa chake kwayo, lakini katikati ya hayo yote, hata mawe yakimpiga pande zote, nyama zikiruka, ngozi ya fuvu la kichwa chake ikiruka, na damu ikibubujika, midomo yake na meno yake yakianguka, hilo lisingeweza kumtenganisha, aliangalia juu na kusema, “Namwona Yesu.”

¹⁶³ Haleluya! Kwa nini? Alikuwa amekuja kwa njia ya Damu, hiyo ndiyo njia pekee ya Mungu ya kuendea. Hata mauti yasingeweza kumtenganisha, mabonge ya mateso, mate, ninii, hakuna kitu kingaliweza kumtenganisha na upendo wa Mungu, alikuwa amepitia njia sahihi, alikuwa amekuja kwa Damu.

¹⁶⁴ Warumi 5:1, ikisema, “Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna amani kwa Mungu.” Ni kitu gani? Ushirika umerejeshwa. Ushirika umerejeshwa tena, amani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. Wakati mwingine tunafikiri ya kwamba watu wa kawaida, kwamba hawastahili, haifai kila- . . . Inastahili kila kitu.

¹⁶⁵ Katika mji ulio karibu nami, majuma machache yaliyopita, lilitukia. Kulikuwako na mzee aliyeishi huko chini kando ya mto, walidhani alikuwa ni ombaomba tu, alisambaza vitini vya kidini. Naye alikuwa . . . Alikuwa amepoteza familia yake, nayo maisha yalionekana kuwa makali sana kwake, naye alikuwa ameipoteza maskini familia yake miaka mingi iliyopita, basi siku moja alikuwa akivuka barabara, ndipo tineja mmoja akaja hapo, mmoja wa hao wahuni, na—na kumgonga yule mzee, akamtupa kando ya barabara, akaivunja mifupa yake yote.

¹⁶⁶ Gari la kuchukulia wagonjwa likamchukua, nao wakampeleka kwenye hospitali ya mji, ndipo wakamfanyia uchunguzi jamaa huyo mzee. Mikono yake ilikuwa imevunjika, mbavu zake zilikuwa zimevunjika, miguu yake ilikuwa imevunjika, naye alikuwa amelala pale mdomo wazi, akionekana amekufa kabisa, amepoteza fahamu.

¹⁶⁷ Na baada ya madaktari kumweka kwenye eksirei na kumwona amevunjika kabisa, walifanya baraza dogo, nao wakasema, “Je, muda wetu unastahili kumshughulikia huyu mzee? Yeye si kitu ila ombaomba.” Kasema, “Itatuchukua saa nyingi, na itachukua *haya* yote, na kila- . . . wakati wengine wanangojea. Naye maskini jamaa huyu ni mzee na—naye ni ombaomba tu, kwa hiyo ha—haingeninii. . . Tusingepata pesa kwake, na—na kamwe haifai kitu. Amevunjika kupita kiasi hata kujaribu bahati naye.” Walikuwa wakifanya baraza.

¹⁶⁸ Huyu mzee hakuwa amekufa kama walivyodhania, waliporudi, na kuanza kumfunika shuka, na kumrudisha tena, alisema, “Hebu kidogo!” Akasema, “Nilisikia mlichosema,” akasema, “Nina thamani fulani, pia.” Akasema, “Mimi nina thamani kubwa sana hata Mungu alimtuma Mwanawe Mwenyewe kufa kwa ajili yangu.” Akasema, “Nilikuwa wa thamani sana hata Mungu akamtoa Mwanawe wa pekee kufa kwa ajili yangu. Miaka hamsini au zaidi, nilikubali jambo hilo lililobarikiwa, niliingia katika ushirika pamoja Naye ambao ni mtamu tu sasa uwezavyo kuwa.” Akasema, “Nina thamani fulani, nina thamani ya kutosha hata Mungu alimtoa Mwanawe kwa ajili yangu.”

¹⁶⁹ Loo, laiti watu wangelitambua thamani ya maisha ya mwanadamu!

¹⁷⁰ Hebu tuangalie ni msalaba wa namna gani, ni gharama ya jinsi gani. Katika kufunga, hebu niseme jambo hili, sikilizeni kwa utulivu, hebu tujipeleke Yerusalemu miaka elfu moja mia tisa iliyopita, na kuilinganisha na bustani ya Edeni. Nitasema ni asubuhi yapata saa moja, ninasikia umati unaoomboleza, ninaenda dirishani pamoja na kusanyiko hili sasa kwa imani, ninainua fre—fremu na kusukuma dirisha nyuma. Kuna nini? Ninaona umbo dogo limeinama chini, namna *hii*, akikokota msalaba mtaani, nao wanampiga mijeledi. Na ma—mate ya dhihaka ya hao askari yametanda usoni Mwake kutokana na kulewa usiku kucha, yananuka.

¹⁷¹ Ninaona taji ya miiba imevutwa kwenye paji la uso Wake, na mchanganyiko wa Damu na machozi. Ninaona joho mwilini Mwake lisilo na mshono ndani yake, doa kubwa mno, nyekundu kote kwenye koti Lake, nao askari wa Kirumi wakimpiga mijeledi wakati akipanda kilima, anakokota akienda. Loo, ni tamasha la jinsi gani! Msalaba huo wa kale ukisugua ngozi kutoka mabegani Mwake anapopanda barabarani. Nao wakimdhihaki, wakipaza sauti, “Salamu, Mfalme wa Wayahudi!”

¹⁷² Lakini ninaona hayo madoa madogo mekundu, yote yanaanza kuwa makubwa zaidi, makubwa zaidi, makubwa zaidi, baada ya kitambo kidogo, yanaingia katika vazi moja kubwa mno, lililolowa damu. Na wakati anapoanza kuipiga miguu Yake anapopanda kilima, Yeye ana—anakaribia sasa kilele cha kilima. Ninamwona nyuki, nyuki anayejulikana sana miongoni mwa jamii ya binadamu aliyeanza kuuma kwenye bustani ya Edeni, anaitwa nyuki wa mauti. Huyu hapa anakuja, anamzunguka mara tatu au nne akilia, ni mauti huku mwiba wake mkubwa umetokeza.

¹⁷³ Akasema, “Unajua nini? Nilifikiri nilipomjaribu kule juu, alishinda majaribu, yeye si kitu ila mwanadamu, huyo asingeweza kuwa ni Mungu. Huyu siye aliyeshuka katika bustani ya Edeni, angesema jambo fulani kulihusu, akiwa na mate hayo usoni mwake. Angewezaje kamwe kujinyenyekeza namna hiyo? Angewezaje kamwe kustahimili mateso? Huyu ni mwanadamu tu. Labda alikuwa ni nabii, hana budi kufa kama watu wengine, kwa hiyo nitamchoma hata afe.” Kwa hiyo yeye anamzunguka-zunguka akilia.

¹⁷⁴ Unajua, ibilisi kamwe hakuamini Yeye alikuwa ni Mungu, daima alidhani Yeye alikuwa ni mwanadamu tu. Ulimwengu wa kidini ulidhani Yeye alikuwa ni laghai, Beelzebuli, mpiga ramli, walimwita hivyo, bali Yeye alikuwa ni Mungu.

Loo, kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,

Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa
chini ya hiyo gharika,
Wanapoteza waa lao lote la hatia.

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahi kuiona
Chemchemi hiyo katika siku zake;
Hapo naomba, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.

Tangu wakati huo kwa imani nilipokiona kijito
hicho
Kinachotolewa na majeraha yako yanayovuja,
Upendo wa kukomboa umekuwa ndio mada
yangu,
Na utakuwa hivyo hata nitakapokufa.

Kisha katika wimbo bora zaidi, mtamu zaidi,
Nitaimba nguvu Zako za kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu unaopiga kithembe,
ugugumizao
Umelala kimya kaburini.

¹⁷⁵ Ee Mwana-kondoo wa Mungu! Huyo hapo anaenda, ibilisi alitoa mwiba wake, huyu hapa anakuja, akivuma karibu Naye, anawazia, “Nitamchoma kwa mwiba wangu, huo utamwondolea mbali, huo utammaliza.” Na baada ya kitambo kidogo, alikuwa, akaamua ya kwamba Yeye hakuwa kitu ila mwanadamu, kwa sababu alidhihakiwa.

¹⁷⁶ Walimfunga kitambaa usoni Mwake apate kuonyesha upambanuzi Wake, walimfunga kitambaa usoni Mwake, na kusema, wakampiga kichwani kwa fimbo, kasema, “Tuambie sasa, wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga. Tuambie ni nani aliyekupiga, tutakuamini sasa. Tutakuamini ukitwambia ni nani aliyekupiga.” Mungu hamfanyii vitimbi mtu yeyote. Alikuwa afanye mapenzi ya Baba.

¹⁷⁷ Ndipo waliposema, “*Ikiwa* wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mkate,” waangalie, ibilisi yule yule usiku wa leo, “*Ikiwa* huu ni uponyaji wa Kiungu, mponye *huyu*.” Unamwona ibilisi yuyo huyo? “*Ikiwa* wewe ni Mwana wa Mungu!”

¹⁷⁸ Huyu hapa huyo nyuki anakuja, mauti, yule adui mkuu wa mwisho wa mwanadamu, akivuma karibu Naye. “Nitamchoma mwiba wangu, na huo utaumaliza.”

¹⁷⁹ Lakini, ndugu, wakati alipochoma mwiba wake katika mwili huo, Huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Kama nyuki akiwahi kuuchoma mwiba wake, mdudu yeyote anayechoma kwenye ki—kina cha kutosha, anapoung’oa, hana mwiba tena, inautoa huo mwiba kwake. Basi wakati huyo nyuki wa mauti alipochoma mwiba wake katika huo mwili wa Mungu pale Kalvari, kuliuchomoa huo mwiba. Haleluya!

¹⁸⁰ Si ajabu Paulo angeweza kusimama na kusema, “Ee mauti, u wapi mwiba wako?” Alipokuwa akijiandaa kukatwa kichwa chake, alisema, “Mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo.”

¹⁸¹ Akasema, “Sikuja kwenu kwa maneno, maneno ya kushawishi na hekima ya wanadamu, ili imani yenu ijengwe katika hekima ya mwanadamu, bali nilikuja kwenu katika nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu.” Huyu mtume mashuhuri Paulo! “Mauti, u wapi mwiba wako?”

¹⁸² Anaweza kuvuma karibu na Mkristo, anaweza kufanya kila namna za mzaha, aseme, “Ah! Nimekupata sasa. Una kansa, una uvimbe, una *huu*, una *ule*, nimekupata sasa.”

¹⁸³ Lakini hebu nikwambie, ndugu, yeye hana mwiba, ana kelele, bali hana mwiba wowote.

¹⁸⁴ Ewe mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe Yule aliyetoa dhabihu kutoka kwenye kutengwa kwake tangu pale mwanzo kwenye bustani ya Edeni, kwamba kupitia Uzao wa mwanamke, kupitia Mwana wa Mungu, Yeye angeung’oa huo mwiba kutoka katika mauti, na kutupa ushindi juu ya kaburi.

¹⁸⁵ Haleluya! Ni njia ya Mungu ya Kiungu ya kuendea, ni njia iliyowekwa na Mungu ya kufanya ushirika Naye.

¹⁸⁶ Ninasema jambo hili moja katika kufunga: Kuna mlango mkubwa mno, mweusi uliowekwa mbele ya kila mmoja wetu, unaitwa mauti, na kila wakati moyo wetu unapopiga, tuko pigo moja karibu zaidi na mlango huo. Nami najua wangu unapiga huko juu, pia. Siku moja utapiga mdundo wake wa mwisho, nami nitaingia. Lakini nitakapoingia, sitaki kuwa kama mwoga, ninataka kujifunika kwa mavazi ya haki Yake, nikijua jambo hili: Kwamba ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake, ya kwamba atakapoita, nitatoka miongoni mwa wafu siku hiyo, nimeoshwa kwa Damu ya Mwana-kondoo, nikisimama, “Sina chochote mikononi mwangu ninacholeta, ninashikilia tu msalabani Pako.”

¹⁸⁷ Sina chochote ningeweza kumpa Mungu, ninaomba tu rehema ya Kiungu na neema. Kupitia Damu ya Yesu Kristo, ninakubali msamaha wangu kwa unyenyekevu, ya kwamba Yesu alikufa mahali pangu, akanitangulia, nami ninaitambua Damu, kwamba aliingia Uweponi mwa Baba huko ng’ambo kuketi kwenye kiti Chake cha enzi, akichukua Damu Yake Mwenyewe na kufanya njia kwa ajili ya mimi na wewe tupate kuendea.

¹⁸⁸ Siionei haya Injili hii ya Yesu Kristo, kwa kuwa ni nguvu za Mungu ziletazo wokovu ninapotembea ulimwenguni nikieneza Damu, na kudai nguvu ambazo Yesu Kristo, aliyefufuka, Yule aishiye, ni yeye yule tu leo kama alivyokuwa jana, na atakuwa

hivyo milele. Mnaamini hilo? Njia ya Mungu ya ushirika ni ipi? Kupitia Damu.

Na tuombe.

¹⁸⁹ Huku vichwa vyenu vimeinamishwa na macho yenu yamefumbwa, sijui jinsi mauti yanavyokuja karibu nanyi, lakini hivi mnamjua Yeye? Si kulijua Neno Lake, si kujua kanuni Zake za imani, si kujua Kanisa Lake, wala kujua watu Wake, lakini je, unamjua Yeye? Je, umekutana Naye binafsi, ukaingia kwenye Damu, katika Utukufu wa Shekina? Kama hujawahi kupitia kwenye Damu, hujui Utukufu wa Shekina, maana Uhai uko tu katika Damu.

¹⁹⁰ Jike halina uhai katika chavua ya jike, ni yai, kiiniyai, bali damu hutoka kwa mwanamume, ambayo ni himoglobini, iliyo katika jinsia ya kiume. Na katika jambo hili, kama hujawahi kuingia kwenye Damu, hujui Uzima ni nini. Je, una ushirika? Au umekuja kwenye maji ya farakano hivi punde tu? Au umeuendea mlango na kutambua kwamba Yeye alikufa kwa ajili yako? Au umeingia ndani?

¹⁹¹ Kama unahitaji vitu hivyo usiku wa leo, waweza tu kuinua mikono yako? Na kusema, “Ndugu Branham, niombe. Sasa nitamkubali katika utimilifu wote wa nguvu Zake, nitamwamini kwa yote yaliyo ndani yangu. Sasa ninakubali hili niingie na ninataka kuingia katika ushirika wa Utukufu wa Shekina, njia iliyowekwa na Mungu. Sioni haya, nitaingia moja kwa moja kwenye chumba cha arusi pamoja na Bwana wangu.”

¹⁹² Utainua mkono wako? Useme, “Nikumbuke katika maombi.” Mungu akubariki, mama. Kunaweza kuwako mwingine? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Je, kunaweza kuwako wengine zaidi ambao wangesema, “Nikumbuke, Ndugu Branham”? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki huko nyuma, naam, mama.

¹⁹³ Kila mtu akiwa ameinamisha vichwa vyao, kila mtu katika maombi aliye kwenye maeneo ya kuombea. Sasa, huenda wewe ni mfuasi mwaminifu wa kanisa, huenda umeishi maisha mazuri, dada, ndugu, bali maisha mazuri hayatafaa kitu, kama yangefanya, ungaliishi kwa sheria; sheria haikumwokoia mtu yeyote, Damu ya Kristo huokoa. Ungeweza kuwa mwanamume mzuri, mwanamke mwema, jirani mwema, mfuasi mzuri wa kanisa, lakini hata hivyo, kama hujaja kwa njia ya Damu, kamwe hujaukaribia ushirika halisi, ushirika halisi wa jamaa na uhusiano, mpaka utakapokuja kwa Damu. Kama ungetaka kukumbukwa sasa, ninakutolea Kristo.

¹⁹⁴ Siku moja. . . Sasa ninasimama kama ndugu kwenu, nami ningewaombea, nifanye lolote niwezalo, Naye anasimama kama Mwokozi wako, leo Yeye ni Mwokozi wako, kesho huenda akawa Hakimu wako. Lakini Yeye ni Mwokozi wako sasa, utaukubali kwa mkono ulioinuliwa? Useme, “Nikumbuke.”

¹⁹⁵ Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki, hapa, Mungu akubariki, mtoto mdogo. Mungu ambariki msichana huyo mdogo. Mungu awabariki wale, huko nyuma, wa—wale mume na mke wakongwe. Mbariki huyu mtu hapa pembeni. Mungu anaiona mikono yenu. Mungu ambariki maskini mvulana huyu mweusi aliyeketi hapa, Mungu awe pamoja nawe, mwanangu.

¹⁹⁶ Akipanda kwenda Kalvari, unajua kilichotukia, mwanangu? Alianguka chini ya huo mzigo, alianguka. Maskini mwili Wake ulikuwa dhaifu sana, asingeweza kusimama tena, ndipo akaanguka, naye Simoni wa Kurene, mvulana mweusi, aliuchukua huo msalaba na kumsaidia kuupandisha kilimani. Huyo alikuwa mmoja wa babu zako, mwanangu. Damu iyo hiyo iliyousugua huo msalaba juu yake inaweza kukujia usiku wa leo, naomba umsaidie kuubeba, mwanangu.

¹⁹⁷ Mtu mwingine? Aseme, “Sasa ninamkubali. Ninataka huyo nyuki asiwe na mwiba wakati daktari anapoondoka kenye kitanda, na kusema hakuna tumaini tena; sitaki mwiba.” Inua mkono wako. Huenda ikaonekana . . .

¹⁹⁸ Unasema, “Inafaa nini kuinua mkono wako?”

¹⁹⁹ Tofauti kati ya mauti na uzima. Kumbuka, sayansi inasema ya kwamba mkono wako hauna budi kuining’inia chini, nguvu za uvutano. Mungu akubariki, huko nyuma, jamaa mdogo. Mungu akubariki, ewe msichana. Hilo ni jema. Hivi, . . . ? Mikono yako huning’inia chini. Mbona usiuihue? Ni kwa sababu una uhai ndani yako, na uhai huo mle ndani, *kitu fulani* kimefanya uamuzi, *kitu fulani* moyoni mwako kimekwambia kuna Mungu, kuna Mtu anayekupenda, kuna Roho karibu nawe. Unaasi kila kanuni ya maumbile unapofanya hivyo, unamwinulia Muumba wako mkono wako, na kusema, “Ninaamini.” Kama unamaanisha hilo, utapita kutoka mautini kuingia Uzamani.

²⁰⁰ Yohana Mtakatifu 5:24 ilisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kuamini,” si kujifanya kuamini, bali anamwamini, “Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele.”

²⁰¹ Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, hiyo ni Roho Mtakatifu. Ingia katika ushirika. Je, kunaweza kuwa na mwingine kabla hatujaomba? Mungu awabariki. Naam, hilo ni sawa, maskini huyu mama hapa.

²⁰² Mpenzi, huenda . . . Mtu fulani huenda akasema wewe ni kijana, yapata umri wa miaka kumi na miwili (Mungu akubariki huko nyuma pia, mwanangu.), sikilizeni, enyi watoto wadogo, Yesu alisema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, Ufalme wa Mungu ni wa walio kama hao.” Hakika, katika siku zako za utotoni sasa, maskini siku zako za ujana, wakati wewe ni . . . barabara ni . . . uko kwenye njia panda hapo, chagua upande unaofaa, nenda pamoja na Kristo. Jambo ndilo hilo.

203 Mtu mwingine kabla hatujafunga sasa? Wanataka kukumbukwa katika maombi. Mungu akubariki huko nyuma, jamaa mdogo. Mungu na akufanye mhubiri. Mungu ambariki mama huyu mweusi aliyeketi papa hapa mbele yangu, dada huyu. Mungu awe pamoja naye. Mungu akubariki, ewe jamaa mdogo, papo hapo. Mtu mwingine, roshani, au mahali popote? Inua tu mkono wako, useme, “Nikumbuke.” Mungu awabariki hawa wote hapa, hilo ni jema.

204 Ninawaona hapa upande wangu wa kushoto, hata kwa watoto fulani wadogo. Mwajua, Maandiko yananena juu ya mtoto mdogo kuwaongoza katika Isaya, mlango wa 10. Mioyo ya—yao haijakokotwa kupitia mambo mengi sana ya ulimwengu, mpaka...wao ni vijana na wachanga, wanampenda Mungu, Mungu anawapenda, na Yeye—Yeye anaweza kuzungumza nao.

205 Tumeona masikitiko mengi sana na kadhalika, ni vigumu kwa mioyo yetu, na mara nyingi tuliipitisha kwenye maskini magazeti ya *Hadithi Ya Kweli* na upuuzi wa ulimwengu, ambayo kamwe hayakupaswa kuwako, yana sugu. Mungu atakuondolea mbali kila sugu ukimruhusu tu akufanye mwororo, mwema, mkarimu, mwenye upendo, mkisameheana, kama tu utakuwa na imani, aminini tu. Ninangojea tu kidogo.

206 Baba yetu wa Mbinguni, ninakuletea kwa unyenyekevu nyara za ujumbe huu mdogo, uliochanganyikana usiku wa leo, hawa watu wa thamani, yapata ishirini ama thelathini waliinua mikono yao, wakisema ya kwamba wanakuhitaji, Ee Mungu, wanataka kuingia kwenye uhusiano na—na kwenye ushirika halisi, wa Kiungu, katika Shekina, Shekina ya Kipentekoste iliyoanguka kwenye Siku ya Pentekoste, ambapo Mungu alishuka, akalipasua lile pazia, na kujileta Mwenyewe mbele ya mwanadamu, kwa sababu Damu halisi ilikuwa imetolewa ambayo ilisamehe dhambi.

207 Damu ya mafahali na damu ya kondoo isingeweza kupachukua mahali hapo, wala haingeweza kumkamilisha mwaminio aliyekuja, kwa sababu uhai uliokuwa katika hiyo damu ulikuwa ni uhai wa mnyama, na uhai wa mnyama haungeweza kuwiana na uhai wa mwanadamu. Lakini wakati yule Mtu alipokuja Ambaye alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, Yeye alikuwa ni Mungu, ndipo basi alipokufa na hiyo Seli ya Damu ikavunjwa, ndipo dhambi ikatalikiwa, dhambi ikaondolewa milele.

208 Sasa tunasimama katika Uwepo wa Utukufu wa Shekina kupitia toleo la Damu Yake inayotusafisha kikamilifu. Naye Roho wa Mungu, kama tujuavyo, aitwaye Roho Mtakatifu, huja na kushirikiana nasi, kwa kuwa Damu inatusafisha na dhambi zote. “Tuna ushirika sisi kwa sisi, wakati Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inatusafisha na dhambi yote.”

209 Jalia kila mmoja walioinua mikono yao usiku wa leo jina lao liwe kwenye kile Kitabu. Jalia waingie katika Utukufu huu mkuu wa Shekina na waokolewe, na wajazwe na Roho, na kuishi pamoja na ushirika mkamilifu hata Kuja kwa Bwana Yesu.

210 Baba, Mungu, hivyo ni kadiri nijuavyo kufanya, ni kuwakabidhi Kwako. Nawe ulisema, "Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu; na Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe." Ulisema utawapa Uzima wa milele na utawafufua katika siku za mwisho.

211 Sasa hawa hapa, kama kumbukumbu za huu Ujumbe ninawakabidhi Kwako, Nawe unawakabidhi kwa Mwana. Na sasa jalia wajazwe na Roho Mtakatifu na waishi kwa furaha, maisha ya mafanikio ya kuwaleta wengine Kwako hata Siku hiyo. Na jalia tukutane nao Utukufuni, waliokombolewa kwa Damu ya thamani ya Mwana-kondoo. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

212 Niliambiwa wakati mmoja na mwanatheolojia mashuhuri, alisema, "Ndugu Branham, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki." Kasema, "Huyu mtu angefanya nini zaidi, ila kuamini?"

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

213 Akasema, "Basi ungewezaje kusema ya kwamba Roho Mtakatifu ni zaidi ya kuamini, kama mtu hawezi kufanya zaidi ya kuamini hata Uzima wa Milele? Ibrahimu aliamini."

214 Nikasema, "Hiyo ni kweli. Lakini Mungu aliitambua imani yake alipompa muhuri wa tohara." Nikasema, "Je, umewahi kuninii. . . kumpokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?"

Akasema, "La, si jinsi unavyoliita pale, kama walivyofanya katika Biblia."

215 Nikasema, "Basi Yeye kamwe hajaitambua imani yako. Anapoitambua imani yako, anakutahiri moyoni, kwa kuingia kwa Muhuri. Nawe unatiwa muhuri na Roho Mtakatifu hata Siku ya Ukombozi wako."

216 Ndugu, dada, Yesu Kristo yupo hapa. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo hapa, Yeye ni Mwokozi, Yeye ni Mponyaji, Yeye ni—Yeye ni Yote katika Yote. Yeye ni Mponyaji kadiri alivyo Mwokozi, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini ya kwamba hii ni kweli, njia ya Kiungu ya kuendea? Mnaamini hilo? Mungu awabariki.

217 Nitawaomba wale walioinua mikono yao waje madhabahuni, kwa dakika moja tu. Lakini kabla hatujafanya hivyo, ni wangapi walio wagonjwa? Hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa, wagonjwa na mnataka Mungu awaponye, inueni tu mikono yenu. Vema.

218 Hatuna kadi za maombi, hawakutoa zozote leo. Huenda kukawa na chache zilizosalia. Baadhi yao...Tuliita watu

kadhaa kutoka yapata saa kumi ama kumi na mbili jana usiku, kwenye yapata ishirini na kitu, ama chochote kile, hakuna mtu aliyekuja, kwa sababu, nadhani, walikuwa wamerudi nyuma kidogo. Hata hivyo, tutazigawa tena kesho.

²¹⁹ Lakini si lazima uwe na kadi ya maombi. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Bwana Yesu Kristo anaweza kushuka na kumtia mtu mafuta hivi kwamba, hata unaweza kugusa vazi Lake? Ni wangapi wanaojua? Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia inasema hivi, ya kwamba “Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu”? Sasa hivi. Na ni vipi Yeye alininii . . . ?

²²⁰ Sasa, mnaamini Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Basi kama Yeye ni yule yule, nawe umguse usiku wa leo, Yeye angetenda vivyo hivyo. Hiyo ni kweli? Sasa, Yeye ni yule yule kwa kila kitu, ila mwili Wake wa kawaida, ameketi mkono wa kuume wa Mungu akituombea tunapokiri. Mnaamini hilo? Ile Damu, Damu Yake Mwenyewe, Yeye alienda kama Kuhani Mkuu kuketi pale, Yeye ndiye anayeweza kuguswa.

²²¹ Sasa, maskini mwanamke mmoja wakati mmoja, labda hakuwa na kadi ya maombi, lakini yeye—yeye alisema, “Ninamwamini Mtu huyo, na kama nikiweza kugusa vazi Lake, nitapona.” Mnaijua hadithi hiyo? Alikuwa akienda zake kumfufua kutoka mautini binti ya Zakayo, ama, binti Yairo.

²²² Kwa hiyo basi angalieni, ndipo maskini mwanamke huyu akajipenyeza katikati ya umati, naye akagusa vazi Lake, ndipo Yesu akageuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Labda watu mara kumi zaidi ya walio hapa usiku wa leo. Ndipo kasema, “Ni nani aliyenigusa?” Hakuna mtu aliyesema kitu, ila Yesu aliangalia kote, akasema, “Nimekuwa dhaifu.”

²²³ Petro akasema . . . Mbona, akamkemea. Hebu tuone kile—tuone kile Petro alichosema, “Bwana, umeingiwa na nini? Ati unasema, ni nani aliyekugusa? Kila mtu anasema, ‘Loo, halo, Kasisi. Hakika tuna furaha kukutana Nawe, tuna furaha Wewe uko katika mji wetu leo, vizuri kukutana Nawe. Tunasikia umekuwa ukifanya mambo makuu, Kasisi.’” Kasema, “Kila mtu anajaribu kukugusa.”

Akasema, “Naam, najua hilo. Lakini mimi . . . Huu ni mguso wa namna nyingine, nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka.”

²²⁴ Ndipo akaangalia kote kwenye kusanyiko, akamwona maskini mwanamke huyo, aliogopa. Labda alikuwa ameketi chini, labda alikuwa amesimama; sikuwako, sijui. Lakini vyovyote alivyokuwa, mahali alipokuwa, Yesu alimwangalia, nguvu za Mungu ndani Yake zikiungana na imani hiyo halisi, akamtambua, akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, na kusema, “Kulikoma. Imani yako imekuokoa.”

225 Sasa nini? Kamwe hakusema, “*Mimi* nilikuokoa, *mimi* nilikuponya.” “*Imani* yako . . .” Neno la Kiyunani hapo ni *sozo*, ambalo linamaanisha “kuokoa,” kama vile kuokoa kimwili, sawa na kuokoa kiroho. Neno lile lile linatumiwa kila wakati. Hiyo ni kweli? *Sozo* ni neno la Kiyunani kwa ajili ya wokovu wa kimwili au wa kiroho pia, *sozo*, neno lile lile. “Imani yako imekuokoa.” Ilikuwa ni kitu gani? Roho wa Mungu ndani Yake.

226 Sasa, ndani Yake mlikaa utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Mnaamini hilo? Vema, ndani yetu mna kijiko kimoja tu chake, kama ile bahari kuu hapa nje, kijiko kimoja tu kutoka baharini. Yeye alikuwa nayo yote bila kipimo, sisi, Biblia ilisema Yeye alikuwa na Roho bila kipimo, tunaye kwa kipimo. Lakini kama nina kijiko kimoja cha maji kutoka baharini, kemikali zile zile zilizoko katika bahari nzima zimo kwenye kijiko hicho.

227 Hiyo ndiyo sababu tuko leo, kama Wakristo, tuko katika ushirika. Ushirika . . . Na Roho yeye yule aliyekuwa ndani ya Kristo yuko ndani ya Kanisa Lake. Kama wewe ni Mkristo, na utaamini kwa moyo wako wote, na kwa imani unyoshe mkono na kumgusa Kuhani Mkuu . . . Na kwenu ninyi waongofu wapya, ambao ndio kwanza mwinue mikono yenu, kuwaonyesha ya kwamba hamjadanganywa, ya kwamba ni Bwana Yesu halisi, kwamba anaishi leo, na ni halisi tu kama alivyowahi kuwa, ombeni.

228 Simjui mtu hapa ndani, sioni mtu mmoja ninayemjua, kumtazama usoni. Wangapi hatufahamiani? Inueni mikono yenu, kwamba mnajua ya kwamba sijui lolote kuwahusu. Vema.

229 Kusanyiko, ninajua nina watu fulani hapa mahali fulani, marafiki fulani, Ndugu Fred Sothmann, na—na ndugu wengine zaidi, Ndugu Dauch, aliyeketi pale pale, na Dada Dauch, ninawajua. Lakini na—nadhani hao ndio pekee, ambao . . . Simwoni hata Ndugu Fred na hao wengine, najua wako hapa mahali fulani.

230 Lakini sikujui, bali Mungu anakujua. Sasa, hebu rudia kisa chako Kwake, na kama Yeye ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, na kama mimi ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake, samahani, neno hilo huwakwaza watu, lakini kama mimi ni mtumishi Wake, nami ninaweza kujitolea kwa Roho Mtakatifu, Yeye atafanya kupitia kwangu vile vile kama alivyofanya kupitia kwa Bwana Yesu. Atatenda kupitia kwako, kama unaweza kuwa na imani ile ile aliyokuwa nayo huyo mwanamke. Unaamini hilo? Kama Yeye ni yule yule.

231 Ni wangapi wanaojua ya kwamba huyo angekuwa ni Mungu? Basi inua mkono wako, useme, “Ninaamini ingekuwa ni Mungu.” Sasa ninyi ombeni, iweni na imani.

232 Hivi mmeshaiona ile picha ya Malaika wa Bwana waliyopiga? Unayo hapa, sivyo, Gene? Imepigwa mara kadhaa. Sasa, Yeye yupo hapa. Nimekuwa nikihubiri juu ya ujumbe wa

wokovu, kwa hiyo nangoja tu kidogo, nikingojea ule upako uje, kumngojea Bwana. Nanyi mlio wagonjwa, kumbukeni tu na mwombe, iweni tu na imani.

²³³ Sema hivi, mwambie Bwana Yesu hivi, useme, “Bwana Yesu, nimemsikia mtu huyo akihubiri hilo, nimesoma hayo katika Biblia. Na—najua yeye hanijui, hajui lolote kunihusu mimi, hajui mimi ni nani, hajui lolote kunihusu mimi, bali ninajua ya kwamba Wewe unanijua. Naye ananiambia ya kwamba Wewe ni yule yule jana na hata milele, ila tu kwamba unatumia miili yetu.” Mungu hutumia miili yetu kama watoto Wake waliofanywa wana wenye mamlaka, kwa neema ya Mungu, kufanya kazi Zake, kama tu vile alivyofanya kupitia Mwanawe wa pekee aliyelipa gharama. “Sasa nena nami kupitia Ndugu Branham, mwambie aniambie jambo fulani, litaniondolea hofu zote na matatizo.”

²³⁴ Kama utakuwa tu na imani na kuamini tu kwa moyo wako wote, Mungu hakika atafanya hivyo. Omba tu, mwangelie Mungu, uwe na imani.

²³⁵ Sasa kwa uchaji kabisa. Maskini mama mmoja ameketi papa hapa, akiomba. Sikujui, hunijui mimi. Una ugonjwa wa moyo, siyvo? Je, una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi. Simama kwa miguu yako kwa dakika moja tu. Vema, kusanyiko, aligusa kitu fulani. Anaagua ugonjwa wa moyo. Hatoki hapa, unatoka Eugene, Oregon. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa wewe rudi nyumbani, na uwe mzima, imani yako inakuokoa.

Unaamini? Sijawahi kumwona huyo mwanamke maishani mwangu. Kuwa na imani.

²³⁶ Huyu hapa mwanamke ameketi hapa ameinua lesa yake, analia. Ameketi hapa mwishoni. Hivi hamwezi kuiona ile Nuru inayoning'inia juu ya yule mwanamke pale? Angalieni hapa. Anaagua ugonjwa wa kifua. Wala hatoki hapa, pia, anatoka California, mji aliotoka unaitwa Eureka, California. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani, dada? Jina lako ni Bi. Wolf, BWANA ASEMA HIVI. Simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, anajua hilo. Rudi nyumbani, dada, Bwana anakuponya.

²³⁷ Kuna mwanamke hapa nyuma kabisa, anaomba. Ameinamisha kichwa chake, analia. Hiyo hapo Nuru ile imesimama moja kwa moja juu ya mwanamke huyo. Ana shida kwenye utumbo mpana, kukakamaa kwa ateri. Jina lake ni Bi. Carrey. Yesu Kristo anakuponya, mama.

²³⁸ Simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu, hatufahamiani kabisa. Kama hiyo ni kweli, mama, inua mkono wako. Imani yako iligusa upindo wa vazi Lake. Amini tu, amini, usitie shaka.

²³⁹ Huyu hapa mtu ameketi, ameketi papa hapa, akiniangalia, ana, kwa namna fulani ni mtu mnene, kidogo anaingia mvi. Ana

koo lenye shida, amefanyiwa upasuaji, huo upasuaji ulikuwa ni kansa, mtu huyo amepoteza sauti yake kutokana nao. Jina lake ni Bw. Lake. Simama kwa miguu yako, Bw. Lake. Pokea uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo.

240 Unaamini? “Kama unaweza kuamini!” Sasa, Roho Mtakatifu yuko tu kote jengoni. Baba yangu wa Mbinguni anajua sijawahi kuwaona wala kuwasikia maishani mwangu, lakini Roho Mtakatifu yupo hapa. Sasa unaamini kwa moyo wako wote?

241 Sasa, kwenu ninyi msiomjua Yeye na mnataka kuingia katika ushirika Wake, kamwe hamtakuwa karibu zaidi Naye mpaka mtakapompata. Mtakuja hapa juu? Mtafikiri Mungu atayasikia maombi yangu? Njoni hapa na msimame, hebu niwaombee papa hapa. Mtakuja? Ninyi nyote mlioinua mkono wenu, mnaweza kuja papa hapa? Simameni hapa kwa muda kidogo tu.

242 Kama atasikia maombi yangu ya kuwaponya wagonjwa, hakika, atasikia kuokoa nafsi. Njoni papa hapa, ninyi mlio na haja Naye sasa hivi, ninawaomba, njoni. Jambo ndilo hilo, njoni moja kwa moja hapa na tuombe. Mungu awabariki. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli.

243 Kuna mtu humu jengoni mahali fulani, ninamwona amesimama mbele yangu, siwezi kutambua mahali walipo. Ni mwanamke, naye anaogua ugonjwa wa jicho, ugonjwa wa ziada, na henia. Bibi Parks, pokea uponyaji wako, Yesu Kristo anakuponya. Um-hum. Hmm!

244 Loo, Yeye ni Mungu. Yeye . . . Roho Mtakatifu yuko miongoni mwa watu hawa. Sasa hilo ndilo . . . Ni wangapi wanaouhisi Uwepo huo? Inua mkono wako. Huo ndio Utukufu wa Shekina, huo ndio ninaozungumzia.

245 Njoo ukiamini. Je, utakuja kuingia katika ushirika huu? Utakuja kwa njia ya Damu usiku wa leo, uje uingie ndani?

246 Ni wahubiri wangapi wa Injili walioko hapa usiku wa leo? Njoni hapa, kwa dakika moja tu. Simameni hapa, ninyi waaminio. Njoni, na tuombe. Njoni mzunguke hapa sasa, simameni, ninyi wahudumu. Ninyi watu mnaomjua Mungu, njoni hapa, na msimame pamoja na watu hawa tunapomba. Ingieni katika Utukufu wa Shekina. (*Kuna Chemchemi Iliyojaa Damu.*)

247 Loo, hii ni halisi. Sasa, huo—huo Uwepo unaouhisi, Uwepo wa Bwana: “Wema huo na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu; nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.” Ee Mungu, ni ajabu jinsi gani! Jambo ndilo hili, rafiki.

248 Sasa ninyi nyote inamisheni vichwa vyenu, na kila mmoja aombe. Ninyi wahudumu, njoni, na msimame karibu na mahali walipo watu hawa wanaokuja, wakitaka Roho Mtakatifu,

wakitaka kuingia. Njoni mzunguke hapa sasa, shukeni mkafanye ushirika. (Njoni, ninawatakeni...?...))

²⁴⁹ Na mara mtakapomkubali Bwana, ninawatakeni... Wahudumu hawa watawapeni nyumbani pa kuja, wawabatize katika ubatizo wa Kikristo, ili kwamba kila kitu kitakuwa sawa kwenu. Wote wanaohusika sasa, tukijua ya kwamba tuko katika Uwepo wa Yesu Kristo...

²⁵⁰ Maskini huyo mama aliyeketi hapa akilia, papa hapa amevaa nguo inayoonekana ya manjano, anaugua ugonjwa huo wa mapindi. Bwana alikuponya, dada. Umekuwa nao kwa muda mrefu, sivyo? Ulikuacha tu wakati huo. Uligusa nini?

²⁵¹ Ni Kuhani Mkuu, ile Nuru, Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli, yeye yule aliyeishi ndani ya Yesu Kristo, Yeye alisema, "Nimetoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu." Paulo alikutana Naye njiani akienda zake Dameski, Naye alikuwa Nuru kuu tena ambayo hata iliyapofusha macho ya Paulo.

Na tuinamishe vichwa vyetu, kila mmoja sasa, tukiimba kwa upole:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Wakati wenye dhambi wakitumbukizwa chini
ya hiyo gharika,
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

²⁵² Kumbukeni sasa, Mungu yupo hapa. Amejithibitisha Mwenyewe kuwa yupo. Kamwe hutakuwa karibu zaidi Naye, mpaka utakapomwona uso kwa uso. Vema.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
hiyo gharika,
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia,
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia;
Na wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya
hiyo gharika,
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

Kila mtu kwa njia yako mwenyewe sasa, omba. Endelea na kinanda chako, ndugu, kwa utulivu, upole.

Tangu wakati huo kwa imani nilipokiona hicho
kijito
Kinachosababishwa na majeraha yako,

²⁵³ Angalia ule msalaba sasa, hapo ndipo alipolipia gharama. Kila mtu hapa ndani akiwa na vichwa vilivyoinamishwa na mioyo iliyoainamishwa mbele za Mungu, tunapoenda kwenye kile Kiti cha Enzi.

²⁵⁴ Baba yetu wa Mbinguni, tunajua ya kwamba Wewe upo. Biblia ni halisi, Mungu wa Biblia yu hai usiku wa leo. Hujafa, bali Wewe u hai milele, u hai milele kutuombea, na umemtuma Roho Mtakatifu arudi, ambapo Wewe ulisema, “Sitawaacha yatima, nitaomba Mtakatifu—Baba Mtakatifu Naye atamrejesha Roho Mtakatifu, Naye atanishuhudia Mimi. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, hata zaidi ya hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²⁵⁵ Huku chini kabisa katika Marekani hii, katika mji huu mdogo wa bonde unaoitwa Klamath Falls, katika Oregon, kwenye bonde la milima hii mizuri, katika jengo hili dogo la shule usiku wa leo, Roho Mtakatifu katika nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo amejidhihirisha Mwenyewe kwa Neno usiku wa leo, na amethibitisha ya kwamba Yeye yu hai milele na milele, na yupo hapa, anaweza hata na zaidi kuokoa kabisa, kuponya maradhi yaliyo mabaya sana, na kumwokoa mwenye dhambi aliyepotea.

²⁵⁶ Mungu, wanaume hawa na wanawake, wavulana kwa wasichana, wamesimama kwa mioyo minyenyekevu katika maungamo, wakitaka kuingia katika utukufu huu, na kupata amani ya Milele daima. Tunawakabidhi Kwako sasa, Bwana. Wamesimama hapa usiku wa leo kama shuhuda. Wewe umesema katika Neno Lako, “Yeye atakayenishuhudia Mimi mbele za watu, huyo nitamshuhudia mbele za Baba Yangu na mbele za Malaika watakatifu. Kama unanionea aibu Mimi na Injili Yangu, nitakuonea aibu Siku ile mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

²⁵⁷ Lakini usiku wa leo, Bwana, wanaume hawa na wanawake, wavulana kwa wasichana wameweka kando aibu yao, wanaingia kwenye chumba cha kulala cha ushirika na uhusiano, wakiomba kwamba Utukufu wa Shekina ushuke juu ya nafsi zao, na kuwabadilisha mbele ya kusanyiko hili, na kufanya viumbe vipya ndani yao. Mungu, ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu ataendeleza kazi hii, na jalia kila mmoja wao apokee baraka ambayo wameijia usiku huu.

²⁵⁸ Umejitalambulisha Mwenyewe, Bwana, kwa nguvu za kufufuka Kwako. Unajua mawazo ya kila mtu. Ulisema hakuna hata shomoro anayeweza kuanguka barabarani, pasipo Baba kujua, na kwa kweli, hiyo ni kweli. Biblia ilisema ya kwamba, “Neno la Mungu lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, huchoma hata kugawanya mafuta ya mfupa, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Kweli, hiyo ni kweli, Bwana.

²⁵⁹ Neno alikuwa... “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye

Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Nalo Neno, usiku wa leo, linaishi miongoni mwetu katika nguvu za Roho Mtakatifu, likipambanua hata mawazo ya moyo.

²⁶⁰ Jinsi tunavyokushukuru Wewe, kwamba katika saa hii kuu, kwamba wakati matumaini yote ya maisha ya kibinadamu yamekwisha, mabomu ya atomiki yamewekwa vibandani, mabomu ya haidrojeni, maradhi na magonjwa, vita vya vijidudu, Ee Mungu, na kila kitu jinsi kilivyo, tukijua ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba wanadamu kwa kweli wataoza miilini mwao, lakini Malaika huyo aliagizwa, “Usiguse yeyote wa hao, usiwakaribie wale walio na divai na Mafuta. Usiwaguse wale walio na muhuri wa Mungu kwenye vipaji vya uso zao.”

²⁶¹ Nasi tunatambua ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ni muhuri wa Mungu, kwa maana imeandikwa katika Waefeso 4:30, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.”

²⁶² Bwana Mungu, litie muhuri kanisa hili usiku wa leo. Wale wanaotaka muhuri wa Roho Mtakatifu, busu kila hofu iondoke, Bwana, na uwatie muhuri kwa muhuri Wako wa Roho mioyoni mwao, hata watatokea kama watoto wachanga waliozaliwa upya, wakilia, “Aba, Baba!” Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu, Mwanao.

²⁶³ Sasa, tunapoendelea kuinamisha vichwa vyetu, kama hutakosa kuamini, bali uamini kwa moyo wako wote, Mungu atakufanyia jambo unalosisama hapa ukilingojea. Sasa tunapomimba tena kwa upole, *Kuna Chemchemi Iliyojaa Damu*, ama, hebu tuabadilishe huo, hebu na tuimbe:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari.

²⁶⁴ Na tuimbe pamoja, huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, tunapomngojea Roho Mtakatifu:

Nampenda, na . . .

²⁶⁵ Loo, enyi marafiki, niaminini, jengo hili limekuwa kama maziwa, Roho Mtakatifu ni halisi sana hapa.

. . .penda . . .

Usiwe baridi, usiwe asiyejali, mchangamkie.

. . .kununua wokovu wangu
Kalvari . . .

²⁶⁶ Sasa, kama hutaamini, kama hutaamini, Yeye hatakuja kwako, lakini kama uko tayari kuachilia kila kitu, Yeye atakuja kwako sasa hivi. Hebu tuuimbe, hebu tuinue mikono yetu, kila mtu sasa.

Na . . .

²⁶⁷ Mnamaanisha kweli? Kama mnalimaanisha, inueni mikono yenu, msemi, “Ninamwamini Yeye.”

²⁶⁸ Vema, Mchungaji, njoo sasa.

... Yeye

Kwani... 

60-0709 Njia Iliyowekwa Na Mungu Ya Kuuendea Ushirika
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org